




**Stars** VS Uganda 'gharika' kwa Mkapa

UKURASA 24


Nipashe
TESA
Jumanne Machi 28, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Afrika Mashariki imo mbioni kuvuna utajiri ndani ya taka za kielektroniki
TEKNOLOJIA
NA GAUDENSIA MNGUMI
MKUTANO KAMALA HARISS, WANASAYANSI
Wabunifu na wagunduzi msiache kitu fungukeni kuendeleza, kuuza juhudi zenu

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Machi 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581263

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US


# Ndugai amvaa Lema

• **Ni** kuhusu kauli yake ya bodaboda... asimulia alivyopitia maisha magumu... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WATANZANIA WAITWA KUCHUKUA VITAMBULISHO NIDA

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewataka Watanzania kwenda kuchukua vitambulisho vyao...





UKURASA WA 3

### KAMALA KUTUA NCHINI KESHO

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, anatarajia kufanya ziara ya siku tatu nchini...

UKURASA WA 4

### MPANGO: KUPANDA MITI NI LAZIMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema suala la kupanda...



## Waandamanaji Kenya wavamia shamba la Uhuru Kenyatta

UKURASA 3



Ndugai   Lema

## Mahakama yataka sheria kufumuliwa

UK. 2

MICHEZO ROBERTINHO: MFUMO SIMBA 'UMETIKI' UK.24 KATUNI UK.6




Mwenyekiti wa Baraza la Usalama Barabarani ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini (kushoto) pamoja na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Ramadhan Ng'azi wakitoa maoni yao mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Hakijinai jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**

# Ndugai amvaa Lema

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge mstaafu, Job Ndugai, amemshukia aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, kuhusu kauli yake ya kudai kuwa kazi ya bodaboda ni laana, huku akieleza alivyopitia maisha ya umaskini.

Ndugai (pichani) amesema anayajua maisha ya umaskini, ameyaishi, amekulia katika hali hiyo tangu anasoma elimu ya msingi hadi anawania nafasi ya ubunge.

Aliyasema hayo juzi kwenye ufunguzi wa mgahawa wa chakula katika eneo la Pandambili wilayani Kongwa mkoani hapo.

"Kazi ni kazi, kikubwa iwe halali, achana naye yule anayesema watu wamelaaniwa sijui wamefanyaje labda amelaaniwa yeye, si yule anayesema vijana wa bodaboda wamelaaniwa si mwendawazimu tu, kazi ni kazi ilimradi iwe halali, we chagua kazi kalaga baho, kama ni mamantilie fanya kazi yako endelea kuikuza utafikia mahali utamiliki hoteli." Alisema Ndugai na kuongeza;

"Bakheresa alianza hana kitu sasa ndiye tajiri na bado anauza maandazi, wengine tatizo kuchagua aina ya kazi, anza huku chini achana na hii sijui ina laana. Wachungaji na mashekhe watatuambia kama ukifanya biashara ya chapati, maandazi au vitumbua au bodaboda zina laana."

### MAISHA ALIYOPITIA

Akielezea maisha aliyopitia, Ndugai alisema ni ya umaskini na anaujua vizuri, kwa sababu ameuishi, ameukulia na huenda jinsi alivyo ni kutokana na hiyo hali.

"Sisi watu wa Kanda ya Kati hapa huwa tunapata tabu ya kujieleza habari ya mali kwa sababu unaona kama watu wataona unatamba kama alivyokumbushia Mkurugenzi tungependa mseme kidogo," alisema Ndugai.

"Na mimi nilipenda niseme kwa sababu kubwa moja kwa vijana wetu angesema hapa tungetokwa na machozi, mimi umaskini naujua vizuri nimeuishi sisimuliwi, nimeukulia na huenda labda hivi nilivyo inatokana na hali hii niliyonayo."

"Nimekulia kwenye nyumba ya tembe, wakati mwingine unakuta mahali mvua ikinyesha mnalala mmesimama kwenye tembe, ukisogea hapa maji, ukisogea pale maji, nimelala chini, nimelalia ngozi, nimeumwa na kunguni, chawa namjua, papasisi namjua, wengine sijui kiswahili nini sinye."

Alisema anajua hali ya kulala njaa kwa sababu amewahi kulala bila kula, amewahi kuchunga mifugo na habari ya kutokula mchana ni jambo la kawaida, ameenda shule kwa kutembea kilomita 16 kwenda na kurudi.

"Kila siku kilomita 16 naenda shule na kurudi, kwa wiki piga hesabu unapata kilomita 80 kwa wiki, hii sio bodaboda na kwa hiyo miaka ambayo nimesoma, umaskini naujua sana siambiwi wala kusimuliwa na mtu.

"Umaskini naujua kwa hiyo hata nilipokuja kuwa mbunge nilizunguka sana tulikuwa na huyu White (White Zubery Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kongwa) tulilala kwenye madarasa, kwenye ofisi za vijiji, kila kijiji tulizunguka na tulilala huko na jioni tuliongea na wazee naifahamu Kongwa maeneo mengine nilikuwa naenda nalia kwanza kwanini niliomba kazi hii ya ubunge, lakini tumepambana sana kwa miaka 20 Kongwa sasa ipo mbali sana."



Anasema la kushangaza akitazama kwenye mitandao ya kijamii mambo mengine moyo wake unauma.

"Lakini nasema Mungu wasamehe kwavile hawajui walitendalo tuna mila na desturi hapa nchini kwetu hatumthamini mwenzetu aliyefanya juhudi akawa tajiri, tunambandika majina freemason, ukiuliza freemason ndiyo nini, hajui, utasikia aah! yule anachinja watu, yule anauza damu, yule alienda kwa waganga, yaani imani haba za ajabu huwezi kuona kwenye mitandao yenu hii hata mara moja wakimpongeza, kumthamini na kumtambua mtu aliyefanya vizuri kiuchumi huwezi kuona."

Hata hivyo, alisema mara kadhaa jimboni mwake wamekuja wakuu wa wilaya wapya na kitu wanachomwambia kuwa yeye ni mtu mbaya sana hafai kabisa.

Amesema wakikaa baada ya miezi sita wanarudi wanasema "mbona tuliambiwa wewe ni mtu mbaya sana nawaambia huwezi kupendwa na watu wote".

### LEMA AMJIBU

Lema akijibu kauli ya Ndugai: "Nimesema umaskini ni laana na ninaomba sana mnisaidie ku-correct (kusahihisha) kwamba bobaboda ni moja ya umaskini mkubwa na ufukara na umaskini ni laana.

"Kuhusu Ndugai anaweza akajua mimi na yeye nani kalaaniwa, lakini akitaka kujua nani kalaaniwa ni yeye alipokuwa anafukuzwa U-spika, aliomba msamaha kama anaomba msamaha mbinguni. Na Biblia imesema amelaaniwa yule amtumainiye mwanadamu, kwa hiyo yeye ana laana kubwa na hiyo laana itamfuata, yuko nayo na atapata majibu muda sio mrefu, naomba niishie hapo."

## Mahakama: Sheria makosa jinai, ushahidi 'zifumuliwe'

**Na Restuta James**

MAHAKAMA imewasilisha maoni kwenye Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki jinai, ikipendekeza 'kufumuliwa' kwa ya sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai sura ya 20 pamoja na sheria ya kutoa ushahidi sura ya sita.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Usimamizi wa Mashauri, Mahakama ya Tanzania, Moses Ndelwa, baada ya kuwasilisha mapendekezo mbele ya Tume hiyo inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Othman Chande.

Alisema nia ya mahakama kutoa uamuzi wa mashauri yanayowasilishwa kwenye mhimili huo na kupendekeza kwamba sheria hizo ziboreshwe ili mashauri yafike mahakamani upelelezi ukiwa umekamilika.

"Mrundikano wa mashauri mahakamani...moja ya sababu ambayo inatufanya tushindwe kutoka hapo ni hizi sheria ambazo sisi hatuna mamlaka nazo," alisema.

"Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ina matatizo makubwa sana, inatakiwa ifanyiwe mabadiliko makubwa sana. Sheria ya Ushahidi ni sheria ya zamani, ya kikoloni ambayo inatakiwa ifanyiwe mabadiliko kwa kiasi kikubwa sana."

Kuhusu upelelezi, alisema mahakama imekwipendekeza kutaka shauri lisiwasilishwe mahakamani kabla upelelezi haujakamilika, akitolea mfano wa kesi za mauaji ambazo zinafikishwa kwenye mahakama za Hakimu Mkazi ambazo hazina mamlaka ya kuzisikiliza, jambo linaloleta usumbufu kwa wananchi.

Ndelwa alisema mapendekezo hayo yanalenga kuwarahisishia wananchi na hususani watuhumiwa wasisote muda mrefu mahabusu au magereza, wakisubiri upelelezi.

Hata hivyo, alisema mahakama inapokea mashauri 200,050 kwa mwaka na kwamba uteuzi wa majaji na kibali cha kuajiri mahakimu 48, kilichotolewa hivi karibuni kimeongeza kasi ya kusikiliza mashauri.

Kadhalika, alisema matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), yamerahisisha utendaji wa mahakama.

Kwa upande wake, Ofisa TEHAMA Mwandamizi wa Mahakama, Samweli Mshote, alisema teknolojia imerahisisha huduma za utoaji haki kwa kuwaunganisha wahusika wote kwa pamoja.

Alisema Mahakama inakusudia kuzindua mfumo wa kesi (case management system), ambayo itaziunganisha idara zote zinazohusika wakiwamo mawakili, magereza, mahakama, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP), Ofisi ya Mwanasheria wa serikali na watuhumiwa.

Alisema mfumo huo utarahisisha usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao na kutoa taarifa za kesi kwa mshataki na mshtakiwa kwa njia ya ujumbe mfupi.

Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, ambaye aliwasilisha maoni ya Baraza la Usalama Barabarani, alisema wamependekeza maboresho kwenye sheria ya usalama barabarani, ili kupunguza ajali.

HABARI KITAIFA

## Waandamanaji Kenya wavamia shamba la Uhuru Kenyatta

**Na Mwandishi Wetu**

MAMIA ya vijana wamevamia shamba linalodaiwa kuwa la familia ya Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta katika eneo la Kamakis, huku maandamano yakiendelea nchini humo kuipinga serikali.

Kiongozi mkuu wa upinzani, Raila Odinga wiki iliyopita aliitisha maandamano kufanyika mara mbili kwa wiki Jumatatu na Alhamisi, kupinga serikali ongezeko la gharama ya maisha na madai kuwa uchaguzi wa 2022 uliibiwa.

Kwa mujibu wa wanahabari wa ndani akiwamo Mwanablogi Pauline Njoroge, kupitia mtandao wake wa Twitter, shamba la Kenyatta limevamiwa na kundi la vijana na kukata miti kwa kutumia misumeno ya umeme na kuiba mamia ya mifugo kwenye shamba hilo kubwa nje kidogo ya Jiji la Nairobi.

"Shamba la Rais mstaafu Uhuru Kenyatta kwa sasa linavamiwa na vijana zaidi ya 1,000. Wamelivamia shamba hilo kupitia upande wa Kamakis," alisema Pauline.

Aidha, ilibainishwa kuwa biashara karibu na shamba lote zilifungwa, pamoja na kiwanda cha gesi kinachomilikiwa na familia ya kiongozi wa upinzani Raila Odinga pia kiliharibiwa katika eneo la viwanda la Nairobi.

Ilibainishwa kuwa maandamano pia yamefanyika katika miji na majiji Magharibi mwa Kenya na katika ngome ya Odinga, waandamanaji walichoma matairi na kuziba barabara kuu katika jiji la Kisumu.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa msafara wa kiongozi wa Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya, Odinga jana ulijitokeza kupitia eneo la Kawangware jijini Nairobi ili kuendeleza maandamano ya pili dhidi ya serikali.

Vyombo vya habari vya ndani vilisema Odinga aliambatana na naibu wake Martha Karua katika muungano huo, kiongozi wa Chama cha Wiper Kalonzo Musyoka na kiongozi wa Chama cha Roots Party, George Wajackoyah.

Ilielezwa kuwa dakika chache baada ya kuanzishwa maandamano hayo huku msafara wa kiongozi huyo ukipenya katika makazi hayo, maofisa wa polisi waliwarushia vitoa machozi waandamanaji waliokuwa wakibeba matawi ya miti, mabango, sufuria na baadhi ya vyakula wakipinga gharama za juu za maisha.

Vile vile, ilielezwa kuwa hatua hiyo ilijiri baada ya Inspekta Mkuu wa Polisi kusema maandamano hayo yalikuwa haramu.

## Kamala kutua nchini kesho

**Beatrice Shayo na Mary Geofrey**

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, anatarajia kufanya ziara ya siku tatu nchini, huku Tanzania ikitarajia kunufaika na mambo mbalimbali ya ujio huo ikiwamo kusainiwa kwa mikataba.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, alisema ziara ya kiongozi huyo itaanza Machi 29 hadi 31.


Alisema ziara hiyo itakuwa ya kihistoria kwa sababu Harris ni mwanamke wa kwanza katika historia ya Marekani kuwa Makamu wa Rais na anatembelea Tanzania ambayo ni nchi ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki kuwa na Rais mwanamke.

Alisema ziara hiyo inafanyika nchini kutokana na mwaliko wa Rais Samia baada ya kukutana na Kamala jijini Washington Aprili mwaka jana alipofanya ziara iliyohusu uzinduzi wa filamu ya kuhamasisha utalii iitwayo Tanzania: The Royal Tour.

Alisema ziara hiyo ni uthibitisho wa uhusiano mzuri kati ya Tanzania na Marekani pia ni matokeo ya juhudi za Rais Samia za kukuza na kuimarisha diplomasia na ushirikiano wa kimataifa.

Alisema baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) atapokewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Machi 30, Rais Samia atampokea Ikulu ya jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo.

Kadhalika, alisema maagizo yaliyotolewa na Bodi ya Shirika la Changamoto za Milenia (MCC) kwa serikali yametekelezwa na kwa sasa mazungumzo yanaendelea vizuri.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa ABSA Group, Arrie Rautenbach, ambao ni wawekezaji wenza na serikali, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Watanzania waitwa kuchukua vitambulisho vyao NIDA

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewataka Watanzania kwenda kuchukua vitambulisho vyao.

Mamlaka hiyo imewataka wafike katika ofisi za mitaa, vitongoji na vijiji, ambako kuna vitambulisho vingi vilivyochapishwa na kupelekwa, lakini havijachukuliwa na wahusika.

Akizungumza na Nipashe jana Msemaji wa NIDA, Godfrey Tengeneza, alisisitiza endapo mwananchi atafika katika ofisi hizo na kukuta kitambulisho chake hakijatoka, aendelee kuvuta subira kwa kuwa mamlaka hiyo inaendelea kuvichapisha hatua kwa hatua.

Alisema kuanzia Machi, 2022 hadi mwaka huu, NIDA imepiga hatua ya kuziunganisha ofisi 142 kati ya 152 za usajili za wilaya, Tanzania Bara na Visiwani na kituo kikuu cha kuchakata taarifa na kwamba ofisi za usajili 17 pia zimeunganishwa na kituo hicho.

"Kwa kawaida fomu na taarifa zinazochukuliwa kutoka kwa waombaji wa vitambulisho vya taifa wakati wa kujisajili ikiwa ni pamoja na alama za vidole, hutumwa kielektroniki kwenda katika kituo cha uchakataji taarifa kwa ajili ya kuendelea na hatua mbalimbali kabla ya kupatiwa kitambulisho.

"Hatua hiyo itawezesha ofisi kutuma fomu na taarifa za usajili za waombaji kielektroniki kutoka katika ofisi hizo za usajili za wilaya kirahisi na kwa haraka zaidi kwenda katika kituo hicho cha kuchakata taarifa," alisema Tengeneza.

Pia hatua hiyo itasaidia kutoa Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) na hatimaye Kitambulisho cha Taifa badala ya kulazimika kwenda kutuma taarifa hizo katika wilaya zilizounganishwa na kituo cha kuchakata taarifa.

Alisema hatua hiyo itasaidia pia maombi ya vitambulisho kutoka kwa wananchi kufika mapema na kwa haraka katika kituo cha kuchakata taarifa na kuongeza kasi ya uchakataji taarifa za waombaji.

Ofisi za wilaya husika zitakuwa na uwezo wa kutuma taarifa hizo kutoka kwenye ofisi zao moja kwa moja.

"Zoezi la uchakataji taarifa linaendelea, usajili ni kitu kinachoendelea siku zote na taarifa pamoja na fomu za usajili hutumwa kielektroniki kila siku kutoka ofisi za usajili, hivyo ambao bado hawajapata vitambulisho waendelee kuwa na subira kwani mchakato unaendelea."

Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP
PO Box 15111, Arusha, Tanzania
www.ujamaa-crt.org

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MKOA WA ARUSHA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MRADI MPYA KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA 2023 MPAKA MWAKA 2025

UCRT KWA UFADHILI WA INTERNATIONAL WORK GROUP FOR INDIGENOUS AFFAIRS (IWGIA) ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA " PROMOTING RIGHTS BASED CLIMATE RESILIENCE WITHIN INDIGENOUS COMMUNITIES " KATIKA WILAYA YA LONGIDO UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 714,636,000

MRADI HUU UITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.

KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tz na manager@ujamaa-crt.or.tz

# Mpango: Kupanda miti ni lazima

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema suala la kupanda miti ni lazima na kuzitaka halmashauri zote nchini kusimamia kwa karibu na kuhakikisha mazingira ya maeneo yao yanakuwa ya kijani, safi, kuvutia na endelevu.

Alisema hayo wakati wa akizindua kampeni ya kupanda miti kitaifa kwa hisani ya Benki ya NMB ikishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), uzinduzi uliofanyika katika eneo la Mtumba jijini Dodoma jana.

Alisema Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini wanapaswa kutoa maelekezo kwa shule, taasisi mbalimbali na kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika uhifadhi na usafi wa mazingira.

Vilevile, Makamu wa Rais ameziagiza halmashauri kwa kushirikiana na TFS, kupanda aina za miti ambayo inaendana na mazingira ya maeneo waliopo pamoja.

Aidha amezielekeza kuziwezesha jamii hususani ya vijana kupata elimu zaidi kuhusu utunzaji wa miti ili kuhakikisha wanachangia katika uhifadhi wa mazingira kwa weledi na kukomesha uvamizi na uharibifu mapori tengefu nchini ili kuboresha hali ya mazingira nchini.

"Hatuwezi kuwa hapa tunalia na vita hii, lakini uvamizi bado unaendelea, serikali ilifanya uamuzi wa makusudi kutengeneza Jeshi Usu, kama nguvu ndogo tuambieni tuwaongezee msaada kutoka kwenye vyombo vingine," alisema.

Aidha aliielekeza TFS kuongeza vitalu vya miche katika maeneo mbalimbali nchini ili wananchi wasihangaike kuitafuta mbali na maeneo yao wakati wa utekelezaji wa upandwaji wa miti hiyo hasa kipindi hiki cha msimu wa mvua.

Alisema pamoja na jitihada za serikali kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi changamoto bado ni kubwa na zinatokana na shughuli za kibinadamu, ikiwamo uharibifu wa misitu, vyanzo vya maji, ukataji wa miti ovyo, tunatupa takataka ovyo, ufugaji na kilimo holela na uvuvi haramu.

Alisema kama kila mmoja atawajibika kwa nafasi yake katika upandaji wa miti dhamira iliyowekwa ni kupanda milioni 1.5 katika kila halmashauri kwa kipindi cha mwaka mmoja itafikiwa.

Alitoa rai kwa Benki ya NMB uwezekano wa kutumia umoja wa benki (TBA) kuongeza nguvu zaidi kuifanya Dodoma kuwa ya kijani kwa muda mfupi zaidi kwa kutambua ndio makao makuu ya nchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alisema ajenda ya upandaji miti nchini ni maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayotaja kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri na miti milioni 40 kwa Mkoa wa Dodoma pekee katika kipindi cha miaka mitano.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema wameelekeza sekretarieti zao zote za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuipa kipaumbele ajenda ya kuhifadhi mazingira katika vikao vyao vyote.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, aliahidi benki hiyo kupanda miti milioni moja kwa mwaka 2023 nchi nzima na kuitunza kuhakikisha inafikia lengo.

Pia, itaendesha shindano maalum la upandaji miti shuleni litakalofahamika kama "kuza miti tukutuze" kupitia shindano hilo litakalofanyika kwa mwaka mmoja na nusu shule zitashindana kutunza miti watakayokabidhiwa na TFS.

Zawadi mbalimbali zitatolewa na shule itakayopanda miti 2,000 na kukuza asilimia 80 na zaidi ya miti hiyo itapata zawadi ya Sh. milioni 50.

Kamishna wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania Prof. Dos Santos Silayo, alisema TFS itashirikiana na NMB kuhakikisha wanatekeleza vema adhma ya upandaji miti milioni moja kwa kutoa miongozo mbalimbali ya kitaalamu na kushirikiana nao katika kila nyanja kuhakikisha adhma hiyo inafanikiwa.

Alitoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kujitokeza kusaidiana na serikali katika kuongeza nguvu kwenye uhifadhi katika kutekeleza kazi mbalimbali zinazopunguza utegemezi wa misitu na hasa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa misitu, upandaji miti na kuhifadhi mazingira.

## Wahoji 'usiri' mchakato Sheria ya Ndoa

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 100 wa kutetea haki za watoto na wanawake (TAPO), wamehoji usiri uliogubikwa katika mchakato wa kubadilisha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Sheria hiyo inaruhusu mtoto chini ya umri wa miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au idhini ya mahakama.

Mwaka 2016, Mkurugenzi wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alifungua kesi ya kupinga vifungu 13 na 17 vya sheria hiyo vinavyoruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa kwa kibali cha mahakana na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi.

Serikali ilikata rufani mwaka 2017, lakini mwaka 2019 Rebeca alishinda baada ya mahakama hiyo kukubali kwamba vifungu hivyo vinapingana na Katiba ya nchi kwa kuweka umri tofauti wa kuolewa kati ya mtoto wa kike na kiume.

Akizungumza kwa niaba ya wadau hao jana kwenye semina na waandishi wa habari Dar es Salaam, Rebeca alisema wanatamani kwamba uamuzi wa mahakama ukazingatiwa na maoni ya wadau.

"Mwaka 2021 serikali ilipeleka muswada bungeni wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa na ulikuwa na makosa mengi. Kwa hiyo wasiwasi wetu ni kwamba kama utarudi kama ule bungeni tutakuwa tunarudi kule kule tulikokataa.

"Hata ule uliopelekwa mwaka juzi bungeni kulikuwa na usiri mkubwa na tulishtukia tu kwamba umepelekwa na ulikuwa na mapungufu mengi na haukuwa umezingatia maoni ya wadau na hukumu iliyotolewa mwaka 2019."

Rebeca alisema katika mswada uliopelekwa na serikali bungeni mwaka 2021 na kurudishwa kwenda kutafuta maoni ya wadau, bado unatoa nafasi kwa mtoto wa miaka 15 endapo mtoto hausiani na mfumo wa shule, idhini ya daktari, Ofisa Ustawi wa Jamii, mzazi, au kama dini inaruhusu.

"Kama mswada utakuwa namna hii, tutakuwa tumerudi kule kule na tutakiwa tumekwenda kinyume na hatujaheshimu uamuzi uliotolewa na mahakama ya rufani wa kuzuia mtoto kuolewa," alisema Rebeca.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akimwagilia maji mti alioupanda, baada ya kuzindua rasmi kampeni ya kupanda miti kitaifa kwa hisani ya Benki ya NMB ikishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), eneo la Mtumba jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

## Watu wawili wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Sumbawanga iliyoketi Mpanda mkoani Katavi imewahukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa watu wawili baada ya kukutwa na hatia ya kosa la kuua kwa kukusudia.

Waliohukumiwa ni Mabula Mwandu (27) na Mwigulu Joseph (25) ambao walidaiwa kumuua kwa kukusudia Maige Makenzi.

Kesi hiyo ilisimamiwa na Wakili wa Serikali, Gregory Muhangwa na kutolewa hukumu na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga, Thadeo Mwenempazi.

Kabla ya hukumu hiyo ilidaiwa mahakamani hapo kuwa chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi.

Ilidaiwa Agosti 30, 2020 katika kijiji cha Urwila Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi washtakiwa wote kwa pamoja walikula njama na kupanga mauaji ya Makenzi.

Siku ya tukio ilidaiwa kuwa marehemu alikuwa amelala chumbani kwake akiwa na mke wake Ester Machia na washtakiwa waliwavamia na kuvunja mlango wao kisha kuingia ndani na kumshambulia Makenzi kwa kutumia silaha za jadi fimbo na rungu hadi kusababisha kifo chake.

Kabla ya kutekeleza mauaji hayo washtakiwa walimtuhumu marehemu kutoka kimapenzi na wake zao.

Akizungumza nje ya mahakama wakili wa upande wa utetezi, Anjela Deus, alisema hawajaridhishwa na hukumu hiyo na ameongea na wateja wake kuwa wanatarajia kukata rufani kupinga maamuzi yaliyotolewa na mahakama hiyo.

**Kabla ya kutekeleza mauaji hayo washtakiwa walimtuhumu marehemu kutoka kimapenzi na wake zao.**



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, Sixbert Jichabu (kulia), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Gas Tanzania, Araman Benoite (wa tatu kulia), wakimkabidhi mtungi wa gesi mjasiriamali Jane Maira wakati wa ugawaji wa mitungi ya gesi na majiko 1,000 kwa wanawake wajasiriamali wa mkoa huo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu awataka wakazi wa Simiyu kutumia fursa SGR

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakazi wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, watumie uwapo wa reli ya kisasa (SGR) kama fursa ya kujijenga kiuchumi.

Alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wananchi na viongozi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Mwenge, Malampaka mjini, wilayani Maswa.

"Hii reli ujenzi wake ni wa viwango, itakuwa na kituo kikubwa sana hapa Malampaka cha kupakia na kushusha abiria, lakini kutakuwa na kituo kikubwa cha kupakia na kushusha mizigo. Halmashauri pimeni ardhi ili wananchi wapate viwanja vya makazi, wapate hati za kufanyia shughuli za maendeleo," alisema.

"Wananchi anzeni kujenga nyumba za kulala wageni ili kituo kitakapokamilika na wageni wakianza kushuka wasilazimike kwenda Mwanza moja kwa moja bali walale hapa watuachie hela. Jengeni hoteli za viwango tofauti," alisisitiza.

Aliwataka viongozi wa wilaya wasiwaache wananchi peke yao bali wawaandalie miundombinu ya ujasiriamali ili kinababa lishe na kinamama lishe wapate maeneo ya kuuzia vyakula vyao kwa ajili ya wageni ambao hawatapenda kula vyakula vya hotelini.

Akijibu hoja ya uhaba wa maji iliyoibuliwa na wananchi hao, Waziri Mkuu alisema Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA) ilishafanya utafiti na kubaini kuwa maji mengi yaliyoko kwenye eneo hilo hayafai kwa matumizi ya binadamu kwa sababu yana chloride nyingi.

Alisema, kutokana na hali hiyo, serikali imetenga Sh. bilioni 22.4 za mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Tabora ambao utapita maeneo hayo na kuwanufaisha wananchi hao.

Waziri Mkuu alikagua ujenzi wa SGR kipande cha tano cha kutoka Isaka hadi Mwanza katika vijiji vya Nyashimba na Badi ambako alielezwa kuwa ujenzi wake umefikia asilimia 28.03.

Akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini (TRC), Mhandisi Masanja Kadogosa, alisema kipande cha Isaka - Mwanza chenye urefu wa kilomita 341 kinajengwa kwa ubia wa kampuni ya CCECC na CRCC zote za China na kitagharimu Sh. trilioni 3.06.

Akitoa mchanganuo wa wafanyakazi waliopo kwenye kipande hicho, alisema hadi sasa mradi wa SGR Lot 5 ulikuwa na wafanyakazi 6,771 na 6,210 sawa na asilimia 91.71 ni Watanzania na 561 sawa na asilimia 8.29 ni raia wa kigeni. "Pia kuna sub-contractors 66 na watoa huduma 337 na hivyo kufanya kiasi cha dola za Marekani milioni 35.4 zibakie kutoa huduma za ndani (local content)," alisema.

Naye Mbunge wa Maswa Magharibi, Mashimba Ndaki, aliishukuru serikali kwa kuweka kituo kikubwa cha kushusha na kupakia abiria hapo Malampaka kwa kuwa anaamini kuwa kitahudumia mkoa huo wa Simiyu, Mara na mji wa Kisumu, Kenya.

"Kikijengwa kituo cha kushusha abiria, na cha kushusha na kupakia mizigo hapa Malampaka, tutafaidika kusafirisha pamba kwa urahisi, lakini tunaomba pia tujengewe pakilio la ng'ombe kwa sababu sisi ni wafugaji na tuna mifugo mingi," aliomba.

Kuhusu sekta ya elimu, Ndaki alisema kwa mwaka huu pekee, wamepatiwa Sh. milioni 660 ambazo zimetumika kujenga madarasa 33. Na katika afya, alisema ndani ya miaka miwili, wamepokea Sh. milioni 400 ambazo zimetumika kujenga zahanati nane. "Pia tumejenga vituo vya afya vya Badi, Shishiu na Zibeya kwa gharama ya Sh. milioni 300, kila kimoja," alisema.

Waziri Mkuu amemaliza ziara ya siku tatu katika Mkoa wa Simiyu ambako alikagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi kwenye wilaya za Itilima, Bariadi na Maswa.



## Wataalamu watakiwa kujadili usimamizi rasilimali bahari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, amewataka watafiti, wataalamu na wanasayansi wa bahari kujadili namna bora ya kutunza, kusimamia na kuwekeza katika rasilimali za bahari nchini ili kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua warsha ya uhakiki wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa awali kuhusu mpango wa matumizi ya maeneo ya bahari (MSP) kwa nchi za Magharibi mwa Bahari ya Hindi iliyoandaliwa na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Maganga alisema kuwapo kwa mpango shirikishi wa matumizi ya maeneo ya bahari ni sehemu ya suluhisho la kuleta matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na kufungua fursa za kiuchumi na ajira kwa kuzingatia utunzaji sahihi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kuna fursa nyingi katika matumizi ya bahari ambazo zikifanyika kwa namna endelevu zitachangia ukuaji wa uchumi. Shughuli kama vile uvuvi mdogo, uvuvi wa bahari kuu, ufugaji samaki na mazao ya baharini zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa buluu na hatimaye kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Alisema Malengo ya Umoja wa Mataifa hasa lengo Namba 14 la Maendeleo Endelevu linasisitiza matumizi endelevu ya bahari.

Maganga alisema mpango huo umekuja katika wakati mwafaka wakati Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, zikiwa zimejipanga kupanua wigo wa matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake ili kujenga uchumi imara.

Kadhalika, mafanikio ya Uchumi wa Buluu yanategemea uwapo wa Mpango Mahsusi wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar zitaendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo.

Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la The Nature Conservancy kutoka Ujerumani, Lucy Maghembe, alisema warsha hiyo imewakutanisha wadau mbalimbali wa masuala ya sayansi ya bahari waliokutana kwa ajili ya kujadili sera na mipango endelevu ya usimamizi wa rasilimali za bahari na namna bora ya kushughulikia migongano ya matumizi ya rasilimali za bahari.

"Katika Afrika Tanzania tunakuwa taifa la nne kuwa na Mpango wa aina hii. Mataifa mengine ya Kenya, Shelisheli na Mauritius zimeanza utekelezaji. Tumejipanga kuja na sera na mipango imara itakayosaidia usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari katika ukanda wa bahari ya Hindi.

Naye Mtaalamu wa Sayansi ya Bahari, Profesa Yunus Mgaya, alisema wanasayansi wamebaini kuongezeka kasi ya matumizi ya rasilimali za bahari katika Ukanda wa Bahari ya Hindi hatua inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za kijamii na kiuchumi ikiwamo nishati, gesi, utalii.

Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Zahor Alharousy, alisema kupitia mpango huo uliobuniwa na wataalamu utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupanua wigo na fursa za ukuaji wa uchumi kwa wananchi hususani wavuvi na wakulima wa zao la mwani.

Tumejipanga kikamilifu kuhakikisha mpango unaondaliwa unakuja na mipango endelevu ya matumizi ya rasilimali za bahari na kuibua fursa kwa wakulima na wavuvi."

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hili la kushusha riba mikopo benki litakomboa wengi

**JUZI** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwaambia wananchi kuwa serikali imeshakaa na taasisi za fedha nchini ili kujadili namna zinavyoweza kupunguza viwango vya riba na makato mengine ili kuwavutia wananchi wengi zaidi kunufaika na huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

Kauli hiyo ya Waziri Mkuu imeleta matumaini kwa wananchi ambao walikuwa wakiogopa kukopa pesa kwenye taasisi za fedha kwa kuhofia riba na badala yake wamekuwa wakitafuta sehemu ambazo wanaweza kukopa kwa riba ndogo.

Suala la riba kuwa kubwa, ndilo lililowafanya watu wengi kuanzisha mifumo isiyo rasmi ya kukopeshana na wengine kuishia kudhulumiwa fedha zao.

Huko mitaani kuna vikundi vingi vimeanzishwa vya kuweka na kukopa ambavyo baadhi yao wananchi huweka fedha zao bila kuwa na uhakika kama zimewekwa mahali salama.

Wengine huanzisha vikundi hivyo kwa kuaminiana tu kwa kumchagua mtu wanayemwona kuwa mwaminifu na kumpa jukumu la kutunza fedha zao mpaka itakapofika wakati wanapotaka kuzikopo.

Kwa kweli utaratibu huu umewaliza watu wengi kwa kuishia kudhulumiwa fedha zao au aliyechaguliwa kuzitunza kudai kuwa ameibiwa. Taasisi za fedha ni sehemu salama ya kutunza fedha, mwananchi ana uhakika kuwa fedha zake ameziweka na mwisho wa mwaka anapata faida kidogo.

Pamoja na kwamba kwenye vikundi wanavyowekeza fedha zao kusaidia kuwakwamua wananchi hao, lakini kama benki zingeweza kutoa mikopo yenye riba nafuu, wengi wangekimbilia kukopa huko na kuachana na vikundi hivyo ambavyo sio salama.

Hata hivyo, vikundi ambavyo mpaka sasa vinafanya vizuri na wanaoweka huko kufanya vizuri ni Vicoba, ambavyo vilipata elimu ya kutunza fedha benki badala ya kuweka kwenye vibubu kama vinavyofanya baadhi ya vikundi.

Vicoba imewakomba kinamama wengi kutokana na kukopeshana katika miradi ya maendeleo mpaka masomo na inapofika mwisho wa mwaka, hugawana faida.

Huu ni mfano wa kikundi ambacho kinaaminika kwasababu kimepata elimu ya kujiendesha na utunzaji fedha unaotambulika. Baadhi ya watu hutumia fursa ya watu kuogopa kukopa fedha benki kwa kuogopa riba kubwa na kuwarubuni kukopa kwenye taasisi zao walizozianzisha kwa kuwapa masharti magumu yakiwamo ya kuchukua kadi zao za benki.

Watu wengine wamepoteza mali zao au kudhulumiwa fedha zao kwa kushindwa kutimiza masharti ya mikopo wanayopewa.

Wengi wanaolizwa ni wastaafu ambao hawakujipanga mapema kimaisha na wanapotoka kazini wanajikuta wana mambo mengi ya kufanya na kuamua kutumbukia kwenye mikopo umiza ambayo uharibu kabisa utaratibu wa maisha yao na wengine kufariki kutokana na msongo wa mawazo.


Suala hili la riba ni muhimu likaangaliwa na kushughulikiwa mapema ili wananchi wasiendelee kudhulumiwa mali zao kutoka kwa watu wajanja wanaojinufaisha kupitia migongo ya wenzao.

Waziri Mkuu Majaliwa aliwahakikishia wananchi kuwa serikali imekuja ikiwa na suluhisho baada ya kubaini kuwa kuna idadi kubwa ya wananchi wanaokwepa kutumia huduma rasmi za kibenki kwa kuhofia ukubwa wa viwango vya riba vinavyotozwa na taasisi hizo na makato mengine.

Ni matumaini yetu kuwa suala hilo litakwenda haraka ili wananchi wanufaike na huduma zinazotolewa na benki zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

### Kama Askofu Malasusa, ukataeni sasa ushoga

**ASKOFU** wa Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania, Alex Malasusa, anawahimiza walimu, wazazi, walezi na viongozi wa dini kuungana kukemea ushoga akikumbusha kuwa wasiiachie serikali yenyewe.

Malasusa, anatoa rai hiyo kwenye maadhimisho ya miaka 30 ya elimu yaliyoandaliwa na Dayosisi ya Mashariki ya Pwani, na kuhudhuriwa na wanafunzi pamoja na wachungaji kutoka makanisa mbalimbali.

Akiwahutubia washiriki, anasema zama hizi ni ngumu, watoto wanaiga mambo kutoka kwenye mitandao ambayo si utamaduni wa Mtanzania.

"Kama unafuatilia habari unasikia mambo ya ovyo yanaigwa kutoka nje na sio utamaduni wetu, na yanaletwa ili tuyazoee vichwani tuone kama kitu cha kawaida, kumbukeni ushoga ni mambo ya kishetani wala hatumung'unyi maneno,"anasema askofu na kuongeza:

"Ni vituko vya ajabu hata wanyama hawafanyi hivyo, nataka wanafunzi wazazi, walezi na walimu mjue kuwa ushoga haumheshimu Mungu. Kama wako waliokengeuka tuendelee kuwaombea wala hatupaswi kuwatuhumu," anakemea.

Askofu Malasusa anatumia mkutano huo kuwaagiza walimu shuleni, vyuoni na ndani ya jamii pamoja na viongozi wa dini mbalimbali kuzuia vitu vinavyoweza kuingia kwenye akili za mwanafunzi na kubadili fikra zao kwa kuiga mienendo isiyofaa kama ushoga.

"Hapa niseme, kutoka wanafunzi wa awali mpaka chuo kikuu ushoga kwetu mwiko, hebu semeni wanafunzi ushoga mwiko. Ukiona mtu anazungumzia hilo chukua jina lake peleka kwa mchungaji au nitakuja mwenyewe. Tena nasikia wachungaji mnasema mnasubiri serikali mpaka itusemee hapana hili ni la kiroho tutapambana nalo wenyewe, tutasimama imara sisi ndio wakupambana". Anasisitiza.

Kukataa ushoga ni jambo linalopaswa kuungwa mkono na kila mmoja kwa vile ni ukweli usiopingika kuwa sio utamaduni wa Mtanzania, lakini kadri siku zinavyosonga mbele kizazi kinazidi kuharibika.

> **Kama unafuatilia habari unasikia mambo ya ovyo yanaigwa kutoka nje na sio utamaduni wetu, na yanaletwa ili tuyazoee vichwani tuone kama kitu cha kawaida, kumbukeni ushoga ni mambo ya kishetani wala hatumung'unyi maneno.**

Hali hiyo, inachangia kuwapoteza wanaume wenye uwezo wa kuzalisha mali, kutunza familia, husambaza magonjwa na kuongeza gharama hasa bajeti ya afya ambayo inaelekezwa zaidi kutibu maradhi yasiyoambukiza kama saratani za njia ya haja kubwa, homa ya ini, kansa za uume na utumbo na mpana.

Mbali na hivyo matendo hayo husababisha kuenea magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake vyote hivyo vikielezwa na wataalamu kuwa husambaa kutokana na kugusa kwa maji maji za mwili zenye virusi.

Kansa ya shingo ya kizazi husambazwa na virusi vya human papilomar virus (HPV) vinavyoelezwa kuwa husambaa kwa njia ya kujamiiana.

Ni vyema pia kukemea na kupiga marufuku biashara za madanguro mitaani na zile za vibanda umiza ambako mbali na kuonyesha burudani vinadaiwa kuhusika na picha za ngono, ubakaji na kulawiti watoto.

Miongoni mwa mambo ambayo mara nyingi huchangia watoto kujiingiza kwenye ushoga ni pamoja na malezi mabovu ya wazazi na walezi ambao hawajali mienendo au mambo wanayofanya au kupitia watoto wao.

Licha ya kuelezwa kuwa ni tamaa za watoto kutaka vitu vya thamani mfano simu, fedha, pikipiki au bajaji za kuwapeleka shuleni ilihali hawana uwezo, tunaamini kuwa mwenye miaka chini ya 18 bado ni mtoto.

Watu wasitumie madai ya tamaa na kuwarubuni watoto badala yake wawaelekeze na kuwasaidia kwa sababu kuharibu na kuwanyanyasa ni kuangamiza Tanzania ya kesho.

Si vyema kuwa na watoto ambao ndiyo viongzi, wataalamu na walipa kodi wa kesho walionyanyaswa kingono kama kubakwa, ulawiti na kujeruhiwa kimwili na kisaikolojia.

Shime kila mmoja asaidie kuwakinga watoto kuiga utamaduni kutoka mataifa mengine kupitia mitandao ya kijamii, sinema, runinga, simu na kompyuta ili wasiangamie.

## HABARI KITAIFA

# Wananchi Isenye wahakikishiwa barabara ya lami

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wananchi wa Isenye, Wilaya ya Serengeti kuzimaliza changamoto zinazoukabili mradi wa ujenzi wa barabara ya Nata - Sanzate (km 40) kwa kiwango cha lami ili iweze kukamilika na kuondoa adha ya usafiri.

Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema hayo wakati akijibu maswali ya wananchi na kuahidi kutoa ushirikiano kwa mkandarasi kwa kuonesha maeneo yote yenye changamoto ili yaweze kutatuliwa kwa haraka ujenzi wa barabara hiyo unapoendelea.

Wananchi hao wameeleza changamoto hizo kuwa ni kusuasua kwa mradi na mkandarasi kutoweka mifereji ya kupitisha maji na kuathiri makazi ya watu.

"Siku zote unapohitaji maendeleo lazima kutakuwa na mabadiliko mengi ya utaratibu wa maisha yaliyokuwepo, na uwepo wa ujenzi wa barabara hii si kukomoa au kuonea watu bali ni kuleta manufaa makubwa na endelevu kwa jamii," alisisitiza Naibu Waziri Kasekenya.

Aidha, amemwagiza mkandarasi kuongeza vifaa, rasilimali watu na muda wa kazi hata kwa kufanya kazi usiku na mchana kwa kuwa wananchi wanahitaji kuona barabara hiyo ikiwa imekamilika.

"Tumemwagiza aongeze wafanyakazi, vifaa na ikiwezekana aongeze shift ili barabara hii ikamilike na ndio kilio cha wananchi hawa kuona barabara inakamilika," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Vicent Mashinji, alimshukuru Naibu Waziri Kasekenya kwa ujio wake katika mkoa huo ambao alisema utaleta msukumo katika ujenzi wa miradi mingi inayoendelea hasa kwa barabara hiyo kuwa ni kiungo muhimu kati ya mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini na nchi jirani ya Kenya.

Akijibu hoja ya wananchi kuhusu uwapo wa mifereji, Meneja wa Wakala ya Barabara (TANROADS), Mkoa wa Mara, Vedastus Maribe, alisema changamoto hiyo anaifahamu na amekwisha mwelekeza mkandarasi kusambaza vifusi vilivyowekwa katika maeneo hasa ya makazi ili kuzuia athari za maji kuingia ndani ya nyumba za watu.

Kuhusu mradi wa barabara hiyo, Maribe, ameeleza mpaka sasa umefikia asilimia 32 na kazi zinazoendelea ni pamoja na kunyanyua tuta la barabara ambalo hadi sasa mkandarasi kafikisha kilomita 23.4 na pia ameshajenga madaraja madogo 45 kati ya 46, madaraja 11 kati 16 na madaraja makubwa amejenga moja kati ya mawili yanayotakiwa.

Alisema gharama ya ujenzi huo ni takribani Sh. bilioni 39 na mkandarasi ni China Railway Seventh Group na kusimamiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Miradi cha Wakala ya Barabara nchini (TANROADS) – TECU.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo amekagua na kuridhishwa na barabara ya Nyamuswa hadi Bulambwa (km 56.4) iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. bilioni 67 zote zikiwa ni fedha za serikali.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, akifafanua jambo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mara, Vedastus Maribe, wakati alipokagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sanzate – Nata (km 40), kwa kiwango cha lami mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yabaini taasisi 10 kutoa mikopo bila leseni

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI binafsi 10 kati ya 15 zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali Manispaa ya Lindi, mkoani hapo, zimebainika kutokuwa na leseni zinazowaruhusu kuendesha shughuli za aina hiyo kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi, Justine Nangu, alibainisha hayo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji kipindi cha miezi mitatu iliyopita, mbele ya waandishi wa habari, mjini humo.

Nangu alisema kutokana na uchunguzi uliofanywa na watendaji wa TAKUKURU katika taasisi hizo zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali wa Manispaa ya Lindi, 10 hazina leseni.

"Sheria inaelekeza wazi taasisi zinazojihusisha na masuala ya kifedha, zikiwamo utoaji mikopo zinatakiwa kuwa na leseni kutoka BoT," alisema Nangu.

Hata hivyo, Nangu hakutaja majina ya taasisi hizo, lakini alisema ufuatiliaji wao, wamebaini watendaji na waendeshaji wa taasisi za utoaji mikopo kutokuwa na taaluma ya fedha, kutoza kiwango kikubwa cha riba, gharama kutokuwa wazi kwa wateja, kuzuia kadi za benki za wateja wanaofika ofisi hizo kuchukua mikopo.

"Tulipowahoji baadhi wamedai wametuma maombi yao BoT, bado majibu hawajarudishiwa na wengine kutokuwa na ufahamu kama wanalazimika kuwa na leseni hizo," alisema Nangu.

Alisema kutokana na mkanganyiko huo, ofisi yake inajipanga kuandaa warsha kujadili matokeo ya uchunguzi wa mfumo huo kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili kupata maazimio yatakayosaidia kutumika kuziba mwanya wa rushwa.

Wakati Mkuu wa Mkoa wa Lindi alipokuwa Nicodemus Banduka, aliwahi kuzifungia taasisi hizo binafsi, kwa makosa mbalimbali yakiwamo kuendesha shughuli bila leseni na tabia ya kuchukua na kukaa na kadi za benki za wateja wao kinyume cha sheria.

## KABWELA



# NALA yapewa leseni mtoa huduma za malipo na BoT

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya teknolojia ya malipo ya nchini Tanzania (NALA), imepokea leseni ya mtoa huduma kwa malipo kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiwa ni matunda ya azma ya Serikali ya Tanzania kuhamasisha uvumbuzi na teknolojia ili kufungua uchumi.

Kampuni hiyo imeidhinishwa na BoT kama mtoa huduma ya malipo, ambayo itawezesha muunganiko wa moja kwa moja na benki pamoja na waendeshaji wa huduma za fedha kwa njia ya mitandao ya simu za mkononi, kama vile Mpesa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mwanzilishi na Mkurugenzi wa Kampuni ya NALA, Benjamin Fernandes, alisema leseni hiyo pia itawezesha kampuni kuanza kutengeneza bidhaa za ziada za kidijitali ambazo zitaongeza ujumuishaji wa malipo, kufanya huduma za malipo ziwe nafuu zaidi na za kuaminika kwa biashara na matumizi ya kawaida.

Alisema NALA ni kampuni ya malipo ya kimataifa iliyozaliwa nchini Tanzania, ilitanua wigo wake kutoka Uingereza na Marekani hadi Ulaya mapema mwaka huu.

"Malengo mawili makubwa ya NALA kutoka mwaka jana yamekuwa kuwezesha ushirikiano wa moja kwa moja kwa benki na kampuni za mawasiliano ya simu, kukabiliana na changamoto ambazo wafanyabiashara wanakabiliana nazo katika kuhamisha fedha kuvuka mipaka ya nchi," alisema.

"Tumefanya kazi kwa karibu pamoja na BoT ili kukamilisha hatua zinazofaa za kupokea leseni yetu kama mtoa huduma wa malipo. Kwa leseni hii mpya mkononi, NALA inapata nafasi na uwezo wa kuendelea na malengo yetu, kubwa likiwa kufanya uwekezaji wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili," alisema.

Alisema NALA inapatikana nchi nyingi za Ukanda wa Afrika na Ulaya, unaweza kuipakua kwenye simu yako kupitia App Store au Play Store.

Alisema licha ya huduma nyingi za kutuma pesa Afrika kutoka ng'ambo, bara hili bado limeendelea kuwa mahali pa gharama kubwa zaidi kutuma pesa.

Alisema NALA ni kampuni ya malipo ya Kiafrika na programu ya kutuma pesa ambayo humwezesha mtumiaji kufanya malipo salama na ya kuaminika kutoka Ulaya, Uingereza na Marekani hadi Afrika kwa sekunde chache.

Alisema kampuni hiyo ina dhamira ya kuongeza fursa za kiuchumi katika bara la Afrika na miongoni mwa wanadiaspora duniani kote.



Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Dk. Harrison Mwakyembe, akizungumza wakati wa kongamano la kupinga ushoga lililojumuisha viongozi wa dini zote lenye kauli mbiu ya "Tanzania bila ushoga inawezekana", jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Wanawake waonyeshwa fursa kujikwamua kiuchumi

**Na Beatrice Shayo**

WANAWAKE wameshauriwa kujikita kwenye masuala ya ugunduzi na teknolojia ili kuwatoa katika wimbi la umaskini na kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Massana, Mary-ani Lema, wakati wa hafla ya taasisi kuadhimisha siku ya kimataifa ya wanawake duniani ambayo hufanyika Machi 8, kila mwaka.

Lema alisema ugunduzi na teknolojia kwa sasa unakua kwa kasi na kurahisisha mambo mengi, hivyo ni muhimu kwa wanawake kujikita katika masuala hayo hasa kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

"Ni lazima kuziba pengo la mgawanyiko wa matumizi ya teknolojia kati ya wanawake na wanaume kwa kuwa katika nyanja hiyo hivi sasa wanawake ni chini ya theluthi moja ya nguvukazi kwenye ajira za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati," alisema.

"Wanawake wote wa Massana tuamke sasa na kushiriki katika ugunduzi na teknolojia, tusijirudishe nyuma kwa kujiona hatuwezi bali tunaweza pasipo kuwezeshwa, tuna imani kuwa mwanamke akiinuka kiuchumi basi familia, jamii na taifa limeinuka,"

Naye Katibu wa Afya katika taasisi hiyo, Alice Baisi, alisema ujasiri na uthubutu katika kujikwamua kiuchumi ni silaha ambazo mwanamke anapaswa kuwa nayo ili kuikomboa familia yake na taifa kwa ujumla.

Alisema ni muhimu kwa wanawake kujitahidi kufanya kazi kwa ujasiri na kujituma kwa kuonesha ubunifu wa kipekee, wasiogope kujifunza au kutoa gharama kwa kuwa kupitia shughuli zao wanatengeneza uhusiano mzuri wa kujitegemea.

# Waliokuwa wafanyakazi Chuo St. John's wadai kuachishwa

**Na Grace Gurisha**

WAFANYAKAZI 21 wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (St. John's University of Tanzania) akiwamo askofu, padri na madaktari wamefungua kesi Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kwa madai ya kuachishwa kazi bila utaratibu.

Amina Sangali na wenzake 20 walifikia uamuzi huo, baada ya chuo hicho kufunga tawi lake lililopo Buguruni Malapa, jijini Dar es Salaam ambalo lilikuwa ni Chuo cha Mapadri (St. Mark's) bila kuwa na barua za kuwaachisha kazi.

Katika hati yao iliyowasilishwa na tume hiyo na Wakili Sylivatus Mayenga, wafanyakazi hao wanaomba Tume ione utaratibu wa kufukuzwa kazi haukuwa sawa, kwa sababu chuo kimefungwa, lakini hawajawahi kupewa barua ya kuonesha ukomo wa ajira zao.

Pia, wafanyakazi hao wanaomba Tume ione kuwa wamejengewa mazingira magumu ya kazi, kwa sababu ya kushindwa kupatiwa kazi za kufanya na kutokulipwa mishahara yao, marupurupu na stahiki zingine.

Novemba 5, 2019 baada ya chuo kufungwa, wafanyakazi 31 wa tawi hilo walipeleka malalamiko yao ya kutolipwa mishahara yao kwa Ofisa Kazi Mfawidhi wa Dar es Salaam, ambaye alitoa uamuzi kwamba mwajiri (St. John's) anatakiwa kuwalipa mishahara yao.

Hata hivyo, chuo hicho hakikubaliana na uamuzi huo uliotolewa Mei 27, 2020 na Yusuph Nzugile, kilikata rufani kwa Kamishna wa Kazi, Ristone Malingumu, lakini kamishna huyo aliendelea kusimamia uamuzi wa Ofisa Kazi kuwa walipwe mishahara yao.

Baada ya uamuzi huo wa Maliamungu alioutoa Julai 24, 2020, Kamishna huyo alipeleka kukazia hukumu mbele ya Msajili wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, Sundi Fimbo dhidi ya St. John's Septemba 6, 2022.

Wakati hatua hiyo inaendelea, St. John's walifungua maombi katika Mahakama hiyo mbele ya Jaji Magimbi dhidi ya St. Mark's na wafanyakazi wakipinga kuwa sio wafanyakazi wao na kwamba suala lililokuwa mbele ya Msajili lisimame hadi kesi hiyo itakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Katika uamuzi wake, Jaji Salma Magimbi alitupilia mbali maombi hayo na hatua ya kukazia hukumu iliyokuwa kwa Msajili ikaendelea, lakini baada ya muda kidogo St. John's wakaomba wafanyakazi hao wakubaliane nje ya mahakama.

Waliingia makubaliano hayo na ya kuyapeleka mbele ya Msajili kwa sababu tayari kulikuwa na kesi, yakasajiliwa mahakamani hapo na St. John's ilikubaliana na wafanyakazi hao kuwalipa mishahara yao kwa awamu tatu.

St. John's walitekeleza makubaliano hayo kwa awamu mbili, awamu ya tatu ambayo ilitakiwa itekelezwe Februari 28, 2023 haijatekelezwa ni madai ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Wengine katika madai hayo ni Askofu Emmaus Mwamakula, Msaidizi wa Askofu wa Mashiriki na Pwani (Anglikana), Richard Kamenya, Kiongozi wa Kanisa la SMC, Padri Lukas Saidi, Kiongozi wa Kanisa la Anglikana Mbweni.

Wengine ni Emmanuel Saninga, Yohana Mtokambali na Samwel Lipembe pia katika madai hayo kuna madaktari ambao ni Dk. Anna Ndebukwa na Dk. Beatrice Halii, Noela Kawia, Michael John, Sophia Msangi, Chard Daniel na wengine wanane.



# Mpango usafirishaji wa dharura wajawazito wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI kwa kushirikiana na Vodacom Tanzania Foundation wamezindua mfumo wa M-mama jijini hapa utakaosaidia upatikanaji wa huduma za dharura za afya kwa wajawazito na watoto wachanga.

Hafla ya uzinduzi wa taasisi hiyo ilifanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mount Meru. Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kituo cha Uratibu wa Rufani na Usafiri wa Dharura cha M-mama kilichopo katika hospitali hiyo, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Arusha, Abel Tupwa, alipongeza mafanikio yaliyopatikana kutokana na mpango huo kwenye kila mkoa.

"M-mama ni matokeo chanya ya ushirikiano wa serikali na sekta binafsi kwa kutoa suluhisho za kibunifu katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii. Mfumo huu unatumia teknolojia rahisi na ya kisasa kuratibu rufani na kuwarahisishia wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga kupata huduma ya usafiri wa dharura ili kuwahishwa kwenye kituo kinachoweza kutoa huduma stahiki," alisema.

Tupwa alisema mfumo huo ukitekelezwa vizuri utapunguza vifo vya kinamama wajawazito na waliojifungua kwa asilimia 38 na watoto wachanga kwa asilimia 47.

"Naomba nitoe wito kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha kuutumia mfumo huu ipasavyo kwani kuna uwezekano mkubwa kila mmiliki wa gari unayemwona mtaani kwako akawa msaada wa kutoa usafiri wa dharura pindi unapopata dharura ya mjamzito aliyejifungua na mtoto mchanga," alisema na kuongeza;

"Lakini pia nawasihi madereva magari binafsi muunge jitihada hizi za serikali na Vodacom katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi mkoani kwetu," alisema.

Mkuu wa Kanda ya Kaskazini wa Vodacom Tanzania Plc, George Venanty, alisema: "Vodacom kwa kushirikiana na serikali, tumetumia ujuzi wetu katika maswala ya teknolojia kuja na mfumo unaoiwezesha serikali kushughulikia dharura na rufaa kwa upesi kwani unawapa uwezo wa kuwaunganisha kinamama wenye dharura au vichanga vyao na magari ya kubebea wagonjwa au madereva jamii."

Alisema utafiti wa majaribio ya mfumo huo ulianza kufanyika katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga mwaka 2013 hadi 2021 ukilenga kutatua tatizo la wajawazito kutokuwa na usafiri na kuchelewa kujifungua.

# Mradi wa afya yangu, mtaji wangu watoa matokeo chanya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAKUNDI sita ya walengwa walioguswa na mradi wa afya yangu, mtaji wangu unaohamasisha matumizi ya huduma mkoba za chanjo ya corona katika Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, umepata matokeo chanya, baada ya kufikiwa watu 662.

Jana Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE CDO linalofanya kazi na makundi ya wananchi wa pembezoni, Aginatha Rutazaa, alisema kuanzia Julai mwaka 2022 hadi Januari mwaka huu, wanajamii hao wameingia kwenye mradi huo moja kwa moja na kupata elimu sahihi na kuingia pia katika chanjo ya corona.

"Wanajamii tuliowagusa na kuanza nao ni watoa maamuzi kwenye ngazi ya jamii, wakiwamo viongozi wa vitongoji, serikali za mitaa, kata; kwa kujua kwamba ndio wenye mamlaka ya kukutana na wanajamii moja kwa moja. Tuliwagusa pia, walioko kwenye maeneo hatarishi kama kundi la waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda. Kundi hili ni kundi ambalo linakaa maeneo ya wazi na wanabeba abiria wa aina mbalimbali na wao ni rahisi sana kupata maambukizi.

**Tangu Julai 2022 hadi kufikia Januari 2023, tumewafikia watu 662, kati yao wanaume ni 113, wanawake ni 332, vijana 199 na watu wenye ulemavu wapatao 18.**

"Wamo vilevile wanafunzi wa vyuo vikuu, ambapo kwa Kilimanjaro, tuna vyuo kama Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini cha Sayansi ya Tiba na Uuguzi cha KCMC, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (MWECAU), Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Stephano Moshi (SMUCo) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Zaidi aliongeza: "Limo pia kundi la jamii ya watu wenye ulemavu, ambalo lina matatizo mara mbili ya wengine, hasa kwa kupata maambukizi ya corona. Tuliona pia tusiwasahau hawa watu wanaofanya tiba asili, kwa sababu dawa za asili hazina thamani kama chanjo ambayo imethibitishwa na Wizara ya Afya nchini na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO). Lakini liko kundi jingine la watu wanaohusika na utoaji huduma za afya katika vituo vya afya kutoa chanjo mkoba."

Awali, Mratibu wa mradi huo, Lawi Msemwa, akizungumza na waendesha bodaboda, alisema mradi huo umejikita katika malengo makuu manne, ambayo ni kuendelea kutoa elimu kwenye jamii kufahamu nini maana ya corona, kujikinga, athari zake na namna ambavyo ugonjwa huo huambukizwa.

Kwa mujibu wa Lawi, lengo la pili ni kuzijengea uwezo kamati za afya za msingi zilizoko ngazi ya vijiji, kuhakikisha kamati hizo zinakuwa na nguvu ya kutoa elimu na lengo la tatu ni kuunga mkono kampeni ya kitaifa ya chanjo salama, ambayo kampeni yake inafanywa na serikali.

Aidha, alisema lengo la nne ni kuunga mkono uhamasishaji wa utoaji wa chanjo kwa njia ya huduma mkoba.

"Tangu Julai 2022 hadi kufikia Januari 2023, tumewafikia watu 662, kati yao wanaume ni 113, wanawake ni 332, vijana 199 na watu wenye ulemavu wapatao 18. Tulianza mradi huu Julai mwaka jana na tunategemea kuhitimisha mradi huu Juni mwaka 2023,"alifafanua.

Katika kikao kazi hicho cha tathmini, Dk. Rennyda Zebedayo kutoka Hospitali ya Manispaa ya Moshi, alisema ni muhimu kwa kila mwanajamii kuchanja kwa sababu ndiyo njia pekee ya kupunguza makali ya virusi vya corona.



Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mount Meru, Shubira Mujuwazi (kushoto), akitoa maelezo kuhusu vifaa vya TEHAMA kwa Ofisa Elimu wa Mkoa Arusha, Abel Tupwa (wa pili kulia), wakati wa ufunguzi rasmi wa kituo cha uratibu wa rufani na usafiri wa dharura cha M-mama, kwa ushirikiano wa serikali na Vodacom Tanzania Foundation mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Vodacom Tanzania Plc Kanda ya Kaskazini, George Venanty (kulia), Mratibu wa Usafirishaji wa hospitali hiyo, Getrude Underson (wa pili kushoto) na Msimamizi wa Programu ya M-Mama kutoka Wizara ya Afya, Jofrey Shayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule za msingi, sekondari zapokea msaada wa chakula

**Na Daniel Sabuni,** MWANGA

SHIRIKA la World Vision, limegawa chakula cha msaada kwa wanafunzi 12,000 wa shule za msingi na sekondari 40 za wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro ili kukabiliana na utoro unaosababishwa na kukosa chakula cha mchana.

Kwa miaka miwili mfululizo sasa, wilaya hizo zinakabiliwa na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Miradi wa World Vision Tanzania, Neserian Mollel, akizungumza jana wakati wa kikao cha uzinduzi wa ugawaji wa vyakula kwa wilaya hizo, alisema chakula hicho kimegharimu zaidi ya Sh. milioni 200.

"Huu ni msaada kutoka Shirika la World Vision Marekani. Mradi huu tutautekeleza kwa kipindi cha miezi mitatu, kuanzia sasa hivi lakini tunaiomba serikali na wadau wengine wajitokeza kuhakikisha watoto wanapata chakula.

"Hatuna uhakika kama mvua zitanyesha za kutosha inavyotakiwa na wananchi watakuwa na chakula cha kutosha. Msaada uliotolewa ni tani 33 za mahindi, maharage na mafuta ya kupikia."

Kwa mujibu wa Neserian, ili kuleta utulivu kwa mtoto darasani na kuwa na uhudhuriaji mzuri shuleni, wameona ni vyema watoto wakapata chakula, kuliko kushinda njaa mpaka warudi nyumbani.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliwasihi wafanyabiashara kuisaidia jamii inayokabiliwa na baa la njaa.

Mkuu wa mkoa huyo alieleza kuwa wanafunzi hao wamekuwa wakishinda na njaa shuleni, lakini hata wakirudi nyumbani hawapati chochote.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdalah Mwaipaya, alisema licha ya wilaya za Mwanga na Same, kukabiliwa na ukame mkali hata mazao kidogo yanayopatikana yamekuwa yakiharibiwa na wanyama kama tembo.





# Dk. Gwajima ataka ushirikiano kudhibiti vitendo vya ukatili

**Na Haloma Ikunji,** SIKONGE

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameitaka jamii kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na kuacha kuwaficha wahalifu wa ukatili huo.

Dk. Gwajima alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea Wilaya ya Skonge na kupokea taarifa ya mwendelezo wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani humo vilivyofikia zaidi ya 180 kwa mwaka.

**Barabara ina urefu wa kilometa 92 na itagharimu zaidi ya Sh. bilioni 152 na ujenzi wake unategemewa kukamilika ndani ya miaka miwili.**

Alisema hali hiyo siyo ya kufumbia macho bali jamii iunge mkono juhudi zinazofanywa na serikali katika kudhibiti vitendo hivyo kwa kutoa taarifa kwa wakati ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua.

"Elimu zaidi iendelee kutolewa ili watu wafahamu madhara ya ukatili wa jinsia na watu waweze kuripoti matukio yanapotolewa hii itasaidia kumaliza vitendo hivi katika jamii zetu," alisema Dk. Gwajima.



Akitoa taarifa ya matukio ya ukatili wilayani humo, Kaimu Ofisa Tawala wa Wilaya ya Sikonge, Rosina Swai, alisema kwa mwaka mmoja matukio yaliyoripotiwa ni 180.

Alieleza kuwa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, ukatili wa kimwili ikiwamo kupigwa ni pamoja na wanawake 87 na wanaume 37 jumla 124 wakati watoto wa kiume watano na wa kike ni 19.

Matukio ya kubakwa na kulawitiwa yameripotiwa wanawake ni 18 na wanaume ni watano, mtoto mmoja aliyelawitiwa na watoto wa kike waliobakwa ni 16.

# Mabinti walioshindwa kuendelea na masomo wapatiwa ujuzi bure

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MABINTI 240 walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupewa ujauzito, wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na wenye ulemavu wamepata fursa ya kusoma katika vyuo vya ufundi bure ili kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa mafunzo VETA, Abdallah Ngodu, aliyasema hayo juzi wakati viongozi wa serikali, mashirika walipotembelea Chuo cha Ufundi Stadi wilayani Kishapu.

Viongozi hao walifuatilia utekelezaji wa mradi wa chaguo langu haki yangu wa kusomesha watoto wa kike mabinti ili watimize ndoto zao.

Mwakilishi kutoka ubalozi wa Finland, Juhana Lethtinen, ambao ndiyo wafadhili wa mradi huo, alisema wamefarijika kuona namna watoto wa kike wanavyopata mafunzo hayo ambayo yatabadilisha mfumo wa maisha yao.

Mshauri wa masuala ya jinsia kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Maya Hansen, aliwataka watoto wa kike hao, kutumia vizuri fursa ambayo wameipata katika kuleta chachu ya mabadiliko katika maisha yao na jamii inayowazunguka.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, ambao ndiyo watekelezaji wa mradi huo kupitia UNFPA, alisema mradi huo ni jumuishi na unahusisha mabinti wenye ulemavu kwa ajili ya kusomeshwa mafunzo ya ufundi stadi bure ili wapate ujuzi ambao utawasaidia kuendesha maisha yao na kuacha kuwa tegemezi.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa kipaumbele katika suala la elimu na kutoa fedha kwa ajili ya kujengwa vyuo vya ufundi stadi ngazi ya wilaya, ambavyo vinasaidia vijana wengi kujikimu kimaisha.



Mabinti wanaoishi katika mazingira magumu, wenye ulemavu na waliokatishwa masomo sababu ya ujauzito, kuolewa ndoa za utotoni, kutoka wilaya za Kahama, Kishapu na Butiama, wakiwa kwenye mafunzo ya kushona nguo ili kutimiza ndoto zao, katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) wilayani Kishapu mkoani Shinyanga jana, yanayotolewa bure kupitia mradi wa "chaguo langu haki yangu" unaotekelezwa na Shirika la WiLDAF, kwa ufadhili wa ubalozi wa Finland kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Majaliwa awacharukia watumishi wanaojifungia ofisini

**Na Alex Sayi,** MASWA

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa (pichani), amewaagiza watumishi wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya kutumia siku nne za kazi kuwahudumia wananchi waliopo vijijini na kuacha utamaduni wa kukaa ofisini wakisubiri ziara za viongozi kuwatembelea wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akihitimisha ziara yake wilayani Maswa mkoani Simiyu na kuwataka watumishi kufanya kazi kwa ajili ya wananchi na siyo kwa maslahi yao wenyewe.

"Nimeshazungumza na watumishi na tayari tumeshakubaliana sasa wawatumikie wananchi kwa kasi kubwa hii itapunguza malalamiko ya wananchi kwa serikali yao," alisema Majaliwa.



Mbunge wa Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, alisema jingo la dharura lililozinduliwa litaweza kuwahudumia wakazi wa Wilaya ya Maswa na wilaya za jirani kwa kuwa lipo kwenye njia kuu inayounganisha wilaya zote za Mkoa wa Simiyu.

Alieleza kuwa katika sekta ya afya vimejengwa vituo vya afya sita na wanaendelea na ukarabati wa zahanati na tayari wamepokea mgawo wa watumishi wa afya 46, lakini kutokana na maboresho na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati wilayani hamo watumishi hao kwa sasa hawatoshi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema kuwa serikali inaendelea kulifanyia kazi tatizo la uhaba wa watumishi wa afya.

Alisema kwa mkoa huo walipokea mgawo wa watumishi wa afya 227 na Wilaya ya Maswa ilipokea watumishi 62 na watumishi 12 wapo katika Hospitali ya Maswa.

Katika hatua nyingine Majaliwa alitembelea kiwanda cha kuzalisha chaki kilichopo maeneo ya Ng'hami wilayani humo kilichojengwa kwa Sh.bilioni nane, huku kiwanda hicho kikiwa kimekamilika kwa asilimia mia.

**Jengo la dharura lililozinduliwa litaweza kuwahudumia wakazi wa Wilaya ya Maswa na wilaya za jirani kwa kuwa lipo kwenye njia kuu inayounganisha wilaya zote za Mkoa wa Simiyu.**

Nipashe
TESA
Jumanne Machi 28, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Afrika Mashariki imo mbioni kuvuna utajiri ndani ya taka za kielektroniki**



Ukurasa 12

Wenye ulemavu miguu wahakikishiwa hawatakwama kuendesha magari



Ukurasa 13

Kumbe inawezekana kote kupikia umeme iwapo tu...

## TEKNOLOJIA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

### MKUTANO KAMALA HARISS, WANASAYANSI

# Wabunifu na wagunduzi msiache kitu fungukeni kuendeleza, kuuza juhudi zenu

'KESHO ni kesho' waandishi mbalimbali kuanzia televisheni za kitaifa na kimataifa, magazeti, redio na mitandao wako Dar es Salaam, ni kwenye mapokezi ya shangwe ya Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris, anayeizuru Tanzania akitokea Ghana.

Ni ziara ya kitaifa itakayokaribisha na kuvuta maofisa, wataalamu na waandishi wa magazeti na vyombo vyote vya habari vikubwa wanaotembea na msafara wa Harris, watakaoshuhudia Watanzania wakimkaribisha mgeni wao kwa bashasha za kila aina kuanzia mavazi, ngoma, nyimbo, michezo , vyakula na vinywaji kwenye dhifa ya kitaifa na popote Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, atakapotembea na mgeni wake.



Rais Samia Suluhu Hassan na  Makamu  wa Rais wa Marekani, Kamala Harris wakiwa katika Ikulu ya White House Washington. Harris anatarajiwa kufika Tanzania kesho akitokea Ghana. **PICHA: IKULU**

Kesho mchana Makamu wa Rais Harris anaondoka Accra Ghana kwenye safari ya saa sita na kuifikia Dar es Salaam, akilitembelea taifa ambalo ni miongoni mwa nchi tatu za Afrika zinazowekeza katika demokrasia, haki za binadamu na maridhiano na hasa wakati huu ambao dunia inakabiliwa na mdororo wa kidemokrasia.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari kutoka mtandao wa Ikulu ya Marekani.

Inasema nchi hiyo inaiona Afrika kuwa muhimu katika kushughulikia changamoto za kimataifa kwa hiyo, ziara ya Mama Harris ni fursa nyingine ya kushauriana na kushirikiana na washirika kuhusu malengo ya pamoja.

Ujio wa kiongozi huyo ni mwendelezo kwa kuwa hapo awali Makamu wa Rais alikutana na viongozi wote watatu wa Afrika ambao anazuru nchi zao huko Washington nazo ni Ghana, Tanzania na Zambia na anatazamia kuimarisha ushirikiano wa Marekani na uhusiano wake na kila mmoja wa viongozi hawa katika safari hiyo.

**AKIWA TANZANIA**

Keshokutwa Alhamisi, anatarajiwa kukutana na Rais Samia, pia anaelezwa kuwa ataweka shada la maua kukumbuka shambulio la bomu katika Ubalozi wa Marekani mwaka 1998.

Baada ya jukumu hilo anakutana na wajasiriamali kwenye viatamizi 'incubators' vya sayansi na teknolojia' kuzungumza nao kuhusu uwekezaji kwenye eneo hilo.

Makamu Harris kutembelea viatamizi ni kipengele kingine muhimu cha safari ambacho kinagusa eneo linalowekwa pembeni la ubunifu na ugunduzi unaofanyika Afrika .

Kuna ubunifu mkubwa lakini kutokana na kukosa fedha hakuna utafiti wala uendelezaji wa sekta hiyo wala sayansi na teknolojia kwa Afrika kwa ujumla.

Ubunifu wa kizawa au 'indegenous' ni muhimu na ndiyo ufunguo wa kutatua kero za jamii kubwa ya bara hilo inayoishi zaidi vijijini kwenye shida ya maji, kilimo cha jembe la mkono, wadudu waharibifu wa mazao, matumizi ya kuni na makazi duni.

Sayansi na ubunifu wa Afrika ukiendelezwa utaleta majibu ya changamoto hizo, badala ya kupachika teknolojia za magharibi.

Ugunduzi wa Afrika unathaminiwa endapo unafanywa kwa kushirikiana na wadau wa nchi zilizoendelea au mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Huu ndiyo wakati wa kufunguka na kuliweka suala la kuendeleza wataalamu wa ndani kwenye ikulu ya Marekani, wakati wa ziara ya Mama Harris.

Taarifa inayoelezea ziara yake, inasema mara nyingi teknolojia za kisayansi na ubunifu unaotokea Afrika hazizingatiwi na watafiti wa kimataifa au wa nje na kwamba safari yake inaweza kusaidia mabadiliko na kuongeza nguvu mpya kwenye sekta hiyo.

Ujio wa kiongozi wa Marekani kwa Tanzania ambayo ni moja ya nchi bora na ya kipekee kuanzia watu, uchumi, rasilimali nyingi, utalii, siasa na juhudi za kufikia maendeleo endelevu Kusini mwa Jangwa la Sahara, unafaa kuiangalia nchi hii kama kiungo cha mataifa sita yasiyo na usafiri wala huduma ya bahari.

Tanzania ni mlango unaoziunganisha nchi za DRC, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Uganda na Bahari ya Hindi ikifungua na kuendeleza uchumi wa nchi hizo kila siku.

Kuimarisha miundombinu, utafiti wa pamoja ili kufikia ubunifu na teknolojia za kisasa za ndani ya mataifa hayo ni suala linalohitaji pia kuishirikisha Marekani.

Kwenye ukanda huo kuna changamoto kama magugu maji ndani ya maziwa, taka za plastiki na za kielektroniki kama vifaa vya kompyuta, simu, rimoti na runinga vilivyosheheni ndani ya maji na ardhini ni suala la utafiti, ubunifu na urejelezaji kuzungumzwa ili kwa pamoja nchi zijinusuru na athari za taka hizo.

Kuna taka za plastiki ambazo zinajaa baharini, ziwani na kwenye mito. Taifa linahitaji kutumia ubunifu na ugunduzi wa ndani wa kufanikisha kuziongezea thamani ikiwa ni pamoja na kuzalisha bidhaa bora zaidi kuanzia mbolea, vifaa vya nyumbani, mapambo na nishati.

Ziara ya Makamu Hariss izungumzie pia jinsi ya kutumia utaalamu wa ndani na kuendeleza juhudi za kupata teknolojia nafuu na ya kifanisi ya kutumia hifadhi ya gesi asilia , upepo, jua na taka ngumu kupunguza uharibifu wa mazingira hasa misitu.

Si vibaya kukumbushia ujio wa Rais Barack Obama, ulioleta pia miradi ya umeme na nishati ukipewa jina la Power Africa.

Power Africa imeshirikiana na

INAENDELEA UK.12

SAYANSI

NA MARY GEOFFREY

# Wenye ulemavu wa miguu waambiwa wasihofu, hawatakwama kuendesha gari



Joseph Sanga.

JOSEPH Sanga ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akisoma shahada ya Uhandisi Mitambo akianza masomo mwaka 2019. Anapomaliza chuo anakuwa mjasiriamali, akifanya ubunifu wa mashine na vifaa vinavyotatua changamoto nyingi zikiwamo za wanaoishi na ulemavu.

Ni kuwatengenezea kifaa rafiki kwenye magari yao ili waweze kuyaendesha kwa wepesi badala ya kukwama kutumia vyombo vya moto na kuendelea na maisha yao kama watu wengine.

Sanga baada ya kumaliza chuo anajiunga na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kuendeleza ubunifu na kwa ushirikiano na wenzake walibuni mashine inayofungwa kwenye gari ili kumwezesha mlemavu, aliyeumia au kupooza miguu, kuendesha gari kwa mikono pekee.

Nipashe inakutana na Sanga jijini Dar es Salaam, kwenye jukwaa linaloandaliwa na Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) linalowaleta pamoja waandishi wa habari za sayansi na teknolojia na watafiti ili kuwajengea uwezo wa kufikisha matokeo ya kazi zao kwa jamii.

Anasema kifaa hicho kinamwezesha mwenye matatizo ya miguu kuendesha gari kama alivyokuwa hapo awali kabla ya kupata matatizo, akiongeza kuwa ni moja ya njia wanayotumia kumsaidia aliyepata ajali kuendelea na shughuli zake ikiwamo kuendesha gari.

"Kwa sababu wapo waliopata ajali wakati wakiwa wanafanya shughuli za kuendesha magari au bajaji nimebuni kifaa ambacho kinatatua changamoto ya mlemavu wa miguu, kuendesha," anasema Sanga.

**UBUNIFU ULIVYOJIBU**

Sanga anaeleza kuwa kifaa hicho ni wazo la muda mrefu na aliliendeleza kwa kubuni njia mbalimbali za kulifanya liwe uhalisia, ili kuwatafutia ufumbuzi wenye ulemavu wa miguu, ili watumie mikono kuendesha magari.

"Nilianza kutengeneza vifaa vya kuunganisha kabla ya kukiunda kifaa au mashine yenyewe na hili nililifanikisha kwa sababu ni kitu ambacho nilifikiri muda mrefu kiwe jibu la watu hawa waliokuwa wanaendesha gari lakini wameacha kwa sababu ya ulemavu," anafafanua zaidi.

Anaongeza kuwa vifaa alivyotumia kuunganisha kupata mashine hizo ni vyuma ambavyo vilianza kuungwa katika mfumo unaomwezesha dereva huyo kutumia mkono na kushika vifaa ambavyo vingeguswa kwa miguu.

Aidha, anasema kifaa hicho kinawekwa kwenye kiti au siti ya dereva ili kukanyaga mafuta na kushika breki kwa kutumia mikono badala ya miguu, na kinaweza kuwekwa na kutolewa kwenye gari bila kuleta madhara kwa mtumiaji.

"Hivyo asubuhi anaweza kutumia mwenye ulemavu kuendesha lakini mchana asiye na changamoto za mahitaji maalumu akikitoa na kuendelea na kazi. Nilikiunda kwa kushirikiana na vijana wenzangu wawili, kilikaguliwa na Jeshi la Polisi kama ni salama, baadaye kikafikishwa Shirika la Viwango (TBS), kwa ajili ya kuanza kutoa huduma rasmi."

Sanga anaongeza kuwa kifaa hicho kinatumiwa kwa magari ambayo ni 'automatic' ambayo hubadilisha gia na breki peke yake unapokanyaga mafuta, wakati ile manual hutamkwa 'manyo'. inayotumia mkono unashikilia na kubadilisha gia na breki kwa mkono.

Anasema kwa usimamizi wa SIDO au kuatamiwa na shirika hilo anafanya ubunifu wa mashine na vifaa vidogo vidogo kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii.

**GHARAMA/USALAMA**

Sanga anataja gharama ya kukifunga kwenye gari kuwa ni Shilingi 600,000 na kufafanua kuwa ni salama kwa watumiaji wa magari, akisema hakina tofauti na mtu anayetumia vifaa vingine halisi vya magari, akiwahakikishia watumiaji kuwa dereva anaweza kukanyaga breki, mafuta na kuendesha gari bila changamoto.

"Kifaa hiki kikifungwa kwenye gari mtu akiwa nje hawezi kuona kuna utofauti wa kutumia mguu na mkono kuendesha gari. Namna ya kuendesha, unaweza kutumia mkono wa kulia au kushoto kutegemea na uhitaji wa mtumiaji. Wengine wanatumia kushoto si kulia hiki kifaa kinaweza kufungwa upande ambao dereva anaweza kuutumia," anasisitiza.

Anafahamisha kuwa mashine hiyo haitumii mafuta wala umeme ili kufanya kazi bali bolti ili kukifunga na haihitaji matengenezo ' service' kwa sababu si ya mafuta wala haigharimu chochote kwenye gari na kuwashauri wenye ulemavu kuzitumia.

Mbali na kifaa hicho Sanga alibuni kifaa cha kunawa mikono kinachokanyagwa kwa mguu ili kupata sabuni na maji bila kushika bomba wala chpa ya sabuni ya maji, akifanya hivyo kabla ya kuwapo kwa tishio la UVIKO-19, na kwamba baada ya kukitengeneza wengi walikielewa lakini hawakuwa tayari kukinunua ila baada ya kutokea UVIKO-19 alizalisha vingi kwa ajili ya kuwekwa kwenye ofisi na maeneo ya mikusanyiko ili watu kunawa na kujikinga na maambukizi ya vizuri hivyo.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, anasema wanashirikiana na wabunifu hao kujenga ili watimize bunifu mbalimbali katika kutoa majibu ya changamoto zilizopo ndani ya jamii.

"Tumewezesha wabunifu wengi kutimiza bunifu zao ambao kwa sasa ni walipakodi wakubwa nchini kama Maxcom Afrika ambaye alipita hapa na sasa yupo Msumbiji na tumeendelea kuwezesha nyingine nyingi," anasema Dk. Nangu.

## WABUNIFU NA WAGUNDUZI MSIACHE KILA KITU FUNGUKENI KUENDELEZA, KUUZA JUHUDI ZENU

INATOKA UK.11

Tanzania kupata nishati za jua, upepo na kusaidia kutatua shida ya umeme kwenye gridi ya taifa, lakini pia ukileta mwanga mpya kwenye uhifadhi wa mazingira na kupunguza uzalishwaji wa hewa ukaa.

Kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani Tanzania inaendelea kufaidika na mkakati wa kukidhi mahitaji ya umeme kwenye gridi ya taifa kwa sababu uzalishaji nishati ulitegemea maji ambao kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa si wa kutegemea tena.

Katika miaka ya hivi karibuni, vyanzo vikuu vya umeme nchini ni gesi asilia na Marekani amekuwa mshirika mkuu mfano, Kinyerezi II inayozalisha megawati 240.

Uzinduzi ukifanyika Aprili 2018 na miongoni mwa wataalamu ni wa washauri wa Power Africa waliofanya mapitio ya kina ya kiufundi ya upembuzi yakinifu wa mradi na kutoa msaada kwa TANESCO kwenye hatua na michakato ya uwekezaji.

Mradi wa Kigoma Solar Power wa megawati 5, ambao ni mtambo wa kuzalisha umeme wa jua huko Kigoma, taifa kwa msaada wa the U.S. Trade and Development Agency USTDA na OPIC na sasa unasambaza umeme kwenye gridi ya taifa.

Kinyerezi I mtambo wa gesi asilia unaozalisha MW 150, kituo kidogo cha kilovolti 132kV na njia za kusambaza umeme za msongo wa 220/kilovolti 132kV ili kuunganisha mtambo mpya wa umeme kwenye mtandao uliopo wa usafirishaji, usingejivunia mafanikio bila msaada wa USAID na kampuni ya Jacobsen Elektro ya Norway.

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Kumbe inawezekana kote kupikia umeme iwapo tu...




Mtendaji Mkuu wa SESCOM Estomih Sawe (kulia) pamoja na maofisa wa kampuni hiyo wakitambulisha majiko sanifu yanayotumia umeme kidogo. **PICHA: SESCOM**

YUNITI ya umeme inauzwa Shilingi 357 wakati kipimo kidogo cha mkaa kinagharamu mpaka Shilingi 2,500 kutegemea mahali unapopatikana. Lakini hakiivishi kilo ya maharage.

Ni ajabu umeme hautumiki kupikia badala yake watu wanapigwa kwenye kuni na mkaa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya SESCOM inayoshughulika na utafiti wa nishati mbadala Estomih Sawe, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam, anasema taifa linaweza kupikia umeme tena kwa tija na unafuu zaidi.

Anasema zinahitajika mbinu na ubunifu kuleta vyanzo nafuu na vyenye ufanisi kwa ajili ya kupikia na SESCOM, imeunda majiko sanifu ya umeme yanayotumia nishati kidogo kupika vyakula vigumu kama maharage na makande kwa muda mfupi na kifanisi.

"Kwa mfano jiko letu linapika kilo ya maharage kwa nusu uniti sawa na Shilingi 146, uniti inauzwa Sh. 357, tena kwa dakika kadhaa. Kama yamelowekwa muda na uniti hupungua zaidi." Anaeleza.

Analinganisha kuwa endapo mpishi atatumia mkaa utagharimu zaidi ya Sh. 3,000 kwa kuwa atahitaji zaidi ya vipimo viwili na muda mrefu pia.

Anaongeza kuwa juhudi za SESCOM zinalenga kutunza mazingira lakini pia kupunguza gharama za kupikia kuni na mkaa ambazo ni kubwa.

Anasema kampuni hiyo imeunda jiko la presha linalotumia umeme linaloitwa JULEP la teknolojia sanifu linalopunguza utegemezi wa kuni na mkaa.

"Teknolojia hii haijajulikana ingawa ni nafuu kuliko kuni, mkaa, mafuta ya taa na gesi za mtungi,"anasema Sawe.

Akifafanua matumizi ya jiko anasema yanaondoa athari kwenye mazingira na kiafya na kusisitiza umuhimu wa serikali na kuondoa kodi, ili majiko haya yauzike kwa bei nafuu na wananchi wengi zaidi wamudu.

"Wananchi wakiyahitaji yanauzwa kwa bei ya punguzo katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Morogoro na Pwani kutokana na ruzuku iliyotolewa na mradi unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya na EU na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (United Nations Capital Development Fund - UNCDF)."

SESCOM inashirikiana na TANESCO wadau wakuu, ili wateja wao watumie jiko hilo, kwa gharama nafuu na linatumia umeme kidogo pia linatunza mazingira, akisema gharama yake inaanzia Shilingi 150,000, anasema.

"Wakati dunia ikipambana kuwapo na ubunifu na matumizi nishati mbadala, ifikapo 2030 lengo namba saba, litatimia tukihakikisha kila mtu anafikiwa na nishati hiyo kwa gharama nafuu," anaongeza Sawe.

Akitoa ufafanuzi zaidi kuhusu jiko hilo, Albina Minja, ofisa wa kampuni hiyo, anasema ni sanifu lililoundwa kwa ufanisi na wakati wa kupikia linaongeza joto lakini baada ya muda linahifadhi joto kali linaloendelea kupika.

"Haliruhusu mvuke kutoka, hivyo joto halitoki nje na chakula huiva kwa mvuke tena lina usalama wa hali ya juu. Tunatoa mafunzo ya namna ya kulitumia kwa usahihi na tunafundisha mafundi, vikundi mbalimbali na mtu ambaye analitumia," anasema Albina.

Kadhalika, Meneja wa kampuni hiyo, Shukuru Meena, anaongeza: "Tunaipongeza serikali kwa kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata umeme. Majiko haya yanatumia umeme kidogo na afya inaboreka, uchumi wa nchi unastawi pia."

Meena anasema wanafanya kampeni za kuelimisha wananchi kuhusu faida za kiuchumi ambazo watapata na kueleza umuhimu wakinababa kuwapa moyo na kuuwaunga mkono kifedha ili kinamama kununua na kutumia jiko hilo, kwa sababu ni rahisi, hawachafuki, wala hawachafui mazingira.

Anaongeza kuwa Tanzania inaweza kuacha kutumia kuni na mkaa na kutumia jiko linalotumia nishati ya jua na kwamba kuna mbadala wa uhakika na endelevu, gharama nafuu kwa kila Mtanzania, kwani taifa linayo nishati na kwamba ukiwa na JULEP huna haja ya kuhangaika kutafuta mkaa na kuni ambazo si salama kwa afya wala mazingira.

### HALI NI MBAYA

Kwa mujibu wa takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, asilimia 85 ya Watanzania wanategemea kuni na mkaa kupikia hatua inayochangia upotevu wa hekta 372,000 za misitu kila mwaka.

Iwapo asilimia hiyo inayofikia watu milioni 52 hupikia kuni na mkaa kupika, ni wazi itafika siku hakutakuwa na mti wala kichaka baada ya miti yote kuwa majivu kwenye majiko ya mijini na vijijini.

Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ya mwaka 2020, inaonyesha kuwa asilimia 63.5 ya kaya zote hutegemea kupikia.

### UMUHIMU WA MAJIKO

Ili kuishi kula ni lazima na mlo hupikwa kwa nishati safi na kwa teknolojia sanifu na endelevu ambayo ni muhimu kwa maisha bora. Lengo namba saba la malengo ya maendeleo endelevu (SDGs-2030) ya Umoja wa Mataifa (UN), ambayo pia ni makubaliano ya mkutano wa Paris, kuhusu kutunza mazingira, huku ripoti mbalimbali zikisema nchi zenye wakazi zaidi ya milioni 55.6 hawatumii nishati na teknolojia za kisasa kupikia.

Sawe analizungumzia hilo akisema walikuja na jiko hilo baada ya kubaini, sehemu kubwa ya kuni na mkaa huwashwa kwenye majiko yasiyo sanifu, mfano kwenye jiko la mafiga matatu kwenye ufanisi wa chini ya asilimia 10.

Jiko hilo ndilo linalotumiwa na asilimia 95 ya Watanzania waishio vijijini na kwamba asilimia 26.2 ya kaya hutegemea mkaa na asilimia 5.1 huitegemea gesi ya mtungi au LPG wakati asilimia tatu pekee hutegemea umeme. Sehemu za mijini kaya nyingi hutumia jiko la bati la mkaa, lenye ufanisi wa chini ya asilimia 15.

### HATUA ZA NCHI

Wastani wa Watanzania 33,000 hufariki kila mwaka, kutokana na moshi wa kupikia, kwa mujibu wa Waziri wa Nishati, January Makamba, anayeeleza hayo jijini Dodoma, Septemba, mwaka jana.

Anatoa takwimu kwenye semina ya kuwajengea uwezo wabunge wanawake kuhusu matumizi ya nishati mbadala nyumbani.

Kwa sasa umeme umefikia asilimia 78.4 ya kaya zote nchini, ingawa kiasi cha watu kinachotumia bado ni kidogo kwa asilimia 37.7, anasema Waziri Makamba.

Kadhalika, umeme katika kaya nyingi unatumika zaidi kwa ajili ya mwanga, kuchaji simu, kuwasha redio, kuangalia televisheni na matumizi mengine madogo, lakini si kupika Makamba anasema.

Aidha, anasema kaya zenye umeme, hununua nishati kama LPG, mkaa na kuni, kwa ajili ya kupikia.

### CHANGAMOTO

Pamoja na faida nyingi zitokanazo na kupika kwa nishati safi ikiwamo ya kiafya, mazingira na uchumi, bado kuna kukwama kufanikisha matumizi mapya.

Ni kutokana na sababu kadhaa kama sera, wafanyabiashara na watumiaji. Sera na mikakati ya kuendeleza nishati na teknolojia za kupika zinapewa kipaumbele kidogo na kutokuwapo bajeti, uwekezaji wa kutosha wa kukuza upatikanaji na matumizi, nacho kikwazo.

Baadhi ya teknolojia za kisasa za kupikia zinaagizwa kutoka nje na kutozwa kodi ya zaidi ya asilimia 40 ya bei ya kununulia na kuzifanya bidhaa hizo, kuwa ghali na kaya nyingi kushindwa kuzimudu.

Zipo teknolojia sanifu kama majiko sanifu ya umeme yenye presha kama vile JULEP, ambayo hayajajulikana sana ingawa ni nafuu kuliko kuni, mkaa, mafuta ya taa na LPG.

Kikwazo ni teknolojia na gharama ya kununulia jiko lenyewe, ambayo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na kuwapo kwa kodi kubwa inayofikia asilimia 46 (VAT 18% kwa mwagizaji na VAT asilimia 18 kwa msambazaji na ushuru wa kuagiza asilimia 10).

TEKNOLOJIA

NA MARY GEOFREY

# Afrika Mashariki imo mbioni kuvuna utajiri ndani ya taka za kielektroniki



BIDHAA za kielektroniki kama kompyuta, simu, rimoti, ving'amuzi, televisheni kamera na betri zina viambato na vifaa ambavyo vinapofikia mwisho wa matumizi vinazalisha taka za kielektroniki.

'E waste' na taka za plastiki si salama kwa mazingira, ni hatari kwa ustawi wa viumbe na mfumo mzima wa ikolojia unaomaanisha maingiliano ya binadamu na mazingira yake wakiwamo viumbe hai walioko angani, ardhini na baharini au majini .

Hata hivyo, utaalamu unawezesha taka hizi za kielektroniki baada ya muda wa matumizi kumalizika tofauti na nyingine zilizozoeleka kwenye mazingira zinaendelea kurejelezwa na hata kutumiwa na mafundi wengine kama vipuri au spea kwa ajili ya kuunda vifaa vingine.

Ripoti ya taifa ya masuala ya taka za kielektroniki ya Tanzania Bara ya mwaka 2019 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaeleza kuwa 2007 zilizalishwa tani 12,500 na miaka 10 baadaye ziliongezeka mara mbili zaidi na kwamba ilipofika 2017 zilizalishwa tani 35,800.

Kwa mujibu wa ripoti ya taarifa kwa umma kuhusu kanuni za udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi ya mwaka 2019 iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, ongezeko la taka za kielektroniki linachochewa na matumizi ya bidhaa za kielektroniki hasa simu, kompyuta, runinga na redio.

Kwa mujibu wa Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP), kila mwaka tani milioni 50 za taka za kielektroniki huzalishwa duniani zikiwa na thamani ya Dola za Marekani bilioni 62 takribani Shilingi trilioni 142.4.

Hata hivyo ni asilimia 20 pekee ya taka hizo za kielektroniki ndiyo hurejelezwa katika mazingira rasmi ili kupata bidhaa mpya bora na zisizo na athari kwa ikolojia.

Katibu Mkuu wa Taasisi ya Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO), Dk. Ally Simba, anabainisha hayo katika kongamano lililojumuisha wadau kutoka nchi saba wanachama, wenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kumaliza tatizo hilo, kuwa wananchi hawana uelewa nini maana ya taka za kielektroniki na madhara yake.

Anasema pia kuna ongezeko la taka nchini kiasi cha tani 17,000 kwa miaka 21 kunakotakana na kungezeka matumizi ya vifaa vya kieletroniki kunakochagizwa na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano.

Anafafanua kuwa vifaa hivyo vinaingia nchini kama misaada lakini kumbe vimekwisha muda wa matumizi hivyo kuwa sehemu ya dampo ya taka hizo.

Katibu Mkuu wa EACO, anataja sababu nyingine kuwa ni vifaa vya kielektroniki vilivyonunuliwa na muda wake wa matumizi kumalizika.

"Kuna ongezeko la kasi, tunaingiza taka za kieletroniki tani milioni 60 kwa mwaka, hivyo mnaona ni nyingi sana kama hakutakuwa na mkakati wa kuzidhibiti," anasema Dk. Simba.

Anafafanua kuwa takwimu za mwaka 1998 zinaonyesha kuwa nchini kulikuwa na tani 2,000 za taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki na hadi kufika mwaka 2019 ziliongezeka na kufika tani 19,000.

Anataja athari za kuwapo kwa taka hizo ni kugeuka kuwa sumu kwa watumiaji wakiwamo watoto wanaozichezea betri na simu za kuchezea.

Anaeleza kuwa kuchanganya taka za kielektroniki na za kawaida kunachafua maji, ardhi na mazingira kwa ujumla kwa sababu zina kemikali hatarishi nyingi na kuongeza kuwa watu bilioni 7.7 duniani hutumia simu za mkononi ambazo zinadumu kwa mwaka mmoja hadi miwili na kugeuka kuwa taka.

Anasema taka za kieletroniki siyo tatizo peke yake bali ni fursa kwa sababu zina madini mengi na kama ukipatikana utaratibu mzuri wa kuzichakata na zinakuwa fursa kwenye biashara.

**UELEWA WA MAFUNDI**

Fundi vifaa vya umeme Jumanne Issa wa Mabibo jijini Dar es Salaam, anazungumza na Nipashe akisema anapokea vifaa kama majagi ya kuchemshia maji, redio na feni, pasi na draya za kukausha nywele saluni.

Anasema: "Baada ya kutengeneza vinavyofaa, vifaa visivyotengenezeka navikusanya na taka nyingine na kuzitupwa dampo. Sijui kama natakiwa kuzipeleka wapi zaidi ya kuzitupa, nyingine zinaonekana lakini zinahitajika kwa sababu kuna vifaa ninavyoweza kutumia kwenye kazi yangu."

Kwa mujibu wa Dk. Simba vifaa vya kielektroniki vilivyotumika vinaweza kwa mara nyingine tena kutumiwa, kuuzwa, kuokolewa, kuchakatwa na kutupwa.

**JUHUDI ZA TCRA**

Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) inayosimamia huduma za mawasiliano inasema kutokana na changamoto hiyo imeweka mikakati ya pamoja ya kuikabili, ni kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari.

Anasema wamekutana wadau mbalimbali wakiwamo watafiti, wataalamu wa mazingira ili kujadili kwa namna gani wanaweza kumaliza tatizo hilo.

Mei mwaka huu, TRCA itaanzisha utaratibu rasmi wa kushughulika na tatizo hilo wakati ambao kampuni binafsi ndizo zinazokusanya na kuziteketeza katika utaratibu bora, anasema na kuongeza kuwa wanashirikiana na nchi wanachama kujadili na kupanga mikakati ya kudhibiti usambaaji kiholela wa e-wastes.

**MSIMAMO WA WIZARA**

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza baada ya kufungua kongamano la wadau wa nchi saba wanachama wa EACO, kujadili na kuweka mikakati ya kumaliza tatizo hilo, anasema ni kubwa linaloendelea kukua ingawa watu wa kawaida hawaoni kwa haraka kwa sababu hawajui pa kuzipeleka.

"Teknolojia inavyoendelea kukua kwa kasi ndivyo vifaa vinavyoonekana vinaanza kupitwa na wakati na kuwa taka, kwa hiyo tunadhani ni muhimu kukutana pamoja na wadau na kuweka namna bora ya kukabili jambo hili," anasisitiza Nape na kuongeza kuwa serikali ina wajibu wa kuweka mikakati ya kumaliza changamoto hiyo.

Anasema pamoja na njia zinazotumika nchini kuharibu taka hizo kupitia kampuni binafsi, bado kuna umuhimu wa kupata nyenzo za kulimaliza tatizo hilo.

MIKAKATI YA EACO

Katika kongamano la EACO lililotanguliwa na mingine minne, umeweka mkakati wa miaka mitano wa kupunguza uwapo wa taka zinazotokana na vifaa vya kielektroniki, anasema Dk. Simba, akisema mojawapo ni kuangalia namna ya kushirikisha watu na kampuni zinazozalisha bidhaa za kielektroniki ambazo vifaa vyake vinakuwa taka kwa kuwatengenezea miongozo na majukumu maalum.

"Pia tumekubadiliana kuendelea kutoa taarifa kwa wananchi, nchi za Afrika Mashariki, zina kamati ya taka za kielektroniki, kupitia hao watakuwa na jukumu la kutoa elimu kwa jamii hasa ya nini wanapaswa kufanya kudhibiti madhara yake ambayo ni hatari kama hazitahifadhiwa kikamilifu," anasema.

Anasema wananchi wanapaswa kutambua kuwa taka za kielektroniki si sahihi kukaa nazo nyumbani, hivyo amewataka kuzipeleka kwenye kampuni na watu wanaokusanya vitu vyote vya kielektroniki ambavyo havifanyi kazi.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Khamis Hamza anasema kupitia EACO, TCRA na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wamewakutanisha pamoja wadau kwa lengo la kuelimishana juu ya namna bora ya kupunguza na kuondoa taka hizo.

"Kutokana na mikataba mbalimbali ambayo serikali imesaini kudhibiti tulipofikia si pabaya sana kwa maana tumeweka msisitizo katika kuelimisha jamii ili kuzuia uwapo wa taka hizi pia kuwafundisha namna bora za kuzihifadhi," anasema.

**ANGALIZO UNEP**

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), linasema taka za kielektroniki ni mbaya na hatari kwasababu haziyeyuki na zinachafua mazingira. Hata hivyo, hivi sasa baadhi ya vijana katika nchi mbalimbali ikiwamo Nigeria wameamua kuwa wabunifu na kugeuza taka hizo kuwa mali.

Jiji kuu la kibiashara la Nigeria taka za elektroniki kwa miaka mingi lilikuwa tatizo sugu, leo zimepata thamani kwa kuchakatwa na kuwa na tija kiuchumi.



## Waziri awaomba viongozi wa dini kutoa elimu kodi ya pango

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amewaomba viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu zaidi kwa Watanzania ili kuona umuhimu wa kulipa kodi ya pango.

Mabula aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini kwenye mahafali ya sita kwa wahitimu wa ngazi ya juu ya madaktari na maprofessa iliyodhaminiwa na Chuo cha Outreach Care International al Marekani yaliyofanyika kwenye Chuo cha Mipango mkoani hapa.

Alisema viongozi wa dini wana uwanja mpana wa kuwaelimisha Watanzania kuhusu ulipaji wa kodi ya pango ambayo kwa hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha wa riba ya kwa wenye madeni.

"Niwaombe viongozi wangu wa madhehebu ya dini endeleeni kuisaidia serikali katika kutoa elimu kwa watu wenu huko kwenye nyumba za ibada kwa ajili ya kulipa hiyo kodi ya pango ambayo imetolewa msamaha na Rais ili Watanzania waitoe bila kushurutishwa,"alisema.

Mkuu wa mafunzo ya viongozi hao waliohitimu elimu ya madaktari na maprofessa, Prof. Rejoice Ndalima aliwataka viongozi wa dini kujiongeza zaidi katika kuitafuta elimu ya kutosha ili kufanya kazi zao vizuri.

Prof. Ndalima alisema wahitimu hao pamoja na viongozi wa madhehebu ya dini wanapaswa kuijenga nchi kwa ajili ya manufaa ya maendeleo ili amani iliyopo idumu kwa Watanzania.

Alisema: "Kama tunataka watu wetu wawe na upendo na uzalendo lazima tuendelea kuimba upendo na amani hapo nchi yetu itakuwa na maendeleo kwa kuwa wananchi wake watakuwa na moyo wa kusameheana na kupendana".

**Viongozi wa dini wana uwanja mpana wa kuwaelimisha Watanzania kuhusu ulipaji wa kodi ya pango ambayo kwa hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa msamaha wa riba ya kwa wenye madeni.**

# RC Singida aagiza wanaoidai h'shauri wapatiwe viwanja

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani humo kutafuta eneo na kupima viwanja ili vigawiwe kwa wananchi wanaodai fidia kwa halmashauri hiyo.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kusomewa taarifa na kamati aliyoiunda kuchunguza migogoro 10 ya ardhi katika Wilaya ya Manyoni.

Katika ripoti ya kamati hiyo iliyosomwa na Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Singida, Shamimu Hoza, ilibainisha kwamba wapo wananchi ambao wanatakiwa kulipwa fidia ya viwanja vilivyochukuliwa na halmashauri hiyo.

**Viwanja hivyo vitagawiwa kwa walengwa kulingana na madai yake na atakaye kataa kupewa kiwanja atapewa fedha za fidia kama ilivyokubalika.**

Kufuatia hali hiyo, Serukamba aliagiza halmashauri hiyo ishirikiane na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mlagaza, pamoja na madiwani wote ili kupata eneo la kuwagawia wananchi na miundombinu muhimu ifikishwe eneo hilo.

Alisema atawasiliana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kutafuta namna ya kupeleka miundombinu hiyo katika eneo litakalochaguliwa na halmashauri hiyo.

Serukamba alifafanua kwamba viwanja hivyo vitagawiwa kwa walengwa kulingana na madai yake na atakaye kataa kupewa kiwanja atapewa fedha za fidia kama ilivyokubalika.

Awali, akitoa taarifa ya kamati Kamishna wa Ardhi mkoani Singida, Hoza alisema migogoro mingi ya ardhi wilayani Manyoni inasababishwa na taasisi zinazohusika kutowasiliana katika umilikishaji wa ardhi na upangaji wa vijiji ambapo vingine vimekuwa ndani ya hifadhi jambo ambalo linasababisha kutokea kwa migogoro.

Aidha, alitoa angalizo kwa wananchi hao kwamba kufyeka pori hakutoi umiliki wa eneo hivyo kila mwenye uhitaji wa ardhi anapaswa kufuata njia zinazostahili ili kupata eneo.

Kamati hiyo ilikuwa ikichunguza migogoro 10 ya ardhi kwenye eneo la viwanja mashamba na mauaji ya wananchi yenye sura ya kishirikina na imani potofu.



Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), Selemani Msuya (kushoto), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Semu Mwakyanjala, kutokana na mamlaka hiyo kufadhili mkutano mkuu wa chama hicho, jijini Dodoma hivi karibuni. Katikati ni Naibu Katibu wa JOWUTA, Said Mmanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maliasili yaagizwa kuweka alama maeneo ya hifadhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeshauriwa kuweka alama kwenye maeneo yote ya hifadhi za kihistoria katika Mkoa wa Dodoma ili kutunza kumbukumbu kwa vizazi vijavyo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na baadhi ya wakazi wa Kikuyu jijini hapo, wakati wakitoa malalamiko ya vivutio vingi vya kihistoria kutelekezwa na havina usimamizi wa moja kwa moja kutoka serikali zaidi ya ule wa kimila, hali ambayo inasababisha uwapo wa shughuli za kibinadamu kufanyika katika maeneo hayo.

Mmoja wa wakazi hao, Johnson Matiko, alisema maeneo mengi yanayobeba historia ya Mkoa wa Dodoma yametelekezwa na kuanza kupoteza uhalisia wake, hivyo alishauri kuwepo namna ya kuweka kumbukumbu ya alama zitakazoonyesha umuhimu wake na kuwa kivutio.

Akitolea mfano wa kivutio ambacho kinatakiwa kuwekwa alama ni eneo lililobeba asili ya jina la Dodoma ambalo tembo alididimia na kuzama na kusababisha wenyeji wa eneo hilo kukiita kitendo hicho Idodomya yaani kudidimia na kusababisha mkoa huo kuitwa Dodoma.

"Mwanzoni eneo hili liliitwa Idodomya lakini kutokana na watalii wa kipindi cha ukoloni kushindwa kutamka neno hilo na kujikuta wakiita Dodoma na hapo ndipo neno hilo likaanza kuzoeleka na kutumika hadi sasa, hii ni historia na ni utalii ambao ukitumika vizuri utaongezea mapato serikali yetu.

"Tunashangaa kuona eneo hili limetelekezwa kiasi hiki mpaka watu wanaanza kujenga majengo yao, kifupi hakuna uhalisia hata mtu akitaka kuonyeshwa alipozama tembo hawezi kuamini, tulitegemea ile juhudi ya Rais katika utalii itaungwa mkono kwa kuweka uhifadhi wa maeneo ya historia ya makao makuu ya nchi lakini bado hakuna utekelezaji,"alisisitiza.

Kiongozi wa kimila wa kabila la wagogo, Chifu Mazengo wa pili alisema kuna haja kwa serikali kuanza upya kutilia mkazo kwa vitendo masuala yote yanayohusu utalii na uhifadhi.

Alisema Mkoa wa Dodoma una vivutio vingi vya kihistoria ambavyo vikiwekewa alama vitakuwa na hadhi na kuvitutia utalii.

Chifu Mazengo alisema: "Vivutio vya asili Dodoma ni vingi lakini utambuzi haupo mfano hapa Kikuyu mbali na kuwepo kwa eneo la tembo, ukiingia ndani ya Chuo Kikuu cha St. John kuna mti mkubwa uliotumika kunyongea wahalifu kipindi cha utumwa lakini ukiwauliza wanaosoma pale hawajui chochote kuhusu mti huo".



HABARI MBEYA

# Wakulima 22,500 kunufaika na elimu ya uboreshaji kilimo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA 22,500 katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma wanatarajiwa kunufaika na elimu ya uboreshaji wa kilimo cha kahawa kwa kuongeza thamani ya zao hilo na kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchini.

Meneja Mradi wa PACE, Amos Mbwambo, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa na Shirika la East and Central Africa (Solidaridad), Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI) na Shirika la Mazingira na Haki za Binadamu (Envirocare).

Alisema unatekelezwa kwa kipindi cha miezi 42 kwa Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Wilaya ya Nyasa na Wilaya ya Mbinga kwa Ruvuma, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa Mkoa wa Songwe ambazo zinalima zao hilo.

**Wanawake wanakabiliwa na ukatili wa kiuchumi ndani ya familia zao.**

Aliongeza kuwa katika mradi huo watawatumia vijana 75 kwa ajili ya kusaidia kuelimisha jamii kuhusu masuala ya jinsia yaliyoibuliwa kwenye utafiti wenye maeneo ya mradi mwaka 2020-2021 na kufundisha vikundi vya wanawake vya kuweka Akiba na kukopa kijijini (KKAKK).

Akizungumzia vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii, Mwanasheria kutoka Envirocare, Godlisten Muro, alisema wanawake wanakabiliwa na ukatili wa kiuchumi ndani ya familia zao.

Alifafanua kuwa wanawake wamekuwa wazalishaji wakubwa wa mazao na shughuli nyingine za kuongeza kipato lakini unapofika wakati wa kufanya maamuzi au kupanga bajeti wanaume hutumia mabavu kumilika rasilimali fedha.

Hivyo, aliwahamasisha wanawake kutofumbia macho vitendo hivyo badala yake wasimame kupigania haki zao pamoja na kuwaelimisha waume zao umuhimu wa ushirikishwaji kwenye kupanga bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

Mkazi wa Kijiji cha Utengule - Usongwe, kilichopo Mamlaka ya Mji mdogo Mbalizi wilayani Mbeya, Rosemary Luvanda, alikiri kuwapo kwa ukatili wa kiuchumi ndani ya familia katika maeneo yao na kwamba wanaume ndio wanaongoza kwa kufanya ukatili huo.

## Wawili mbaroni tuhuma ya unyang'anyi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, linawashikilia watuhumiwa wawili Mussa Mapunda (38), Patrick Samwel (36) wakazi wa Airport ya zamani kwa tuhuma za unyang'anyi wa kutumia silaha aina ya panga.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi ACP, Benjamini Kuzaga, watuhumiwa hao walikamatwa Machi 20, mwaka huu baada ya kufanya msako maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema awali Machi 18, 2023 maeneo ya Ituha jijini Mbeya Lusubilo Lucas (45) Mwalimu wa Shule ya Msingi Inyala alivamiwa na kundi la vijana na kisha kumjeruhi kichwani na kumpora pikipiki yake na kukimbia.

Alisema baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya lilianza msako na hatimaye Machi 20, 2023 maeneo ya Ilomba jijini Mbeya lilifanikiwa kuwatia mbaroni watuhumiwa wawili kwa tuhuma za kuhusika katika tukio hilo.

"Watuhumiwa wanaendelea kuhojiwa ili kubaini mtandao mzima wa matukio ya unyang'anyi na uporaji na baada ya upelelezi kukamilika watafikishwa mahakamani," alisema ACP Kuzaga.

Aliongeza kuwa katika mwendelezo wa misako hiyo, Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa sita kwa tuhuma za wizi katika maduka ya bidhaa mbalimbali na kwa mawakala wa fedha.

Watuhumiwa waliokamatwa ni Fatuma Abubakari (60), Lukresia Raurent (48), Aselina Juma (26), Mohamed Abubakari (52), Toni Silvester (37), Fanuel Mzava (40) wote wakazi wa Soweto mkoani Kilimanjaro walikamatwa wilayani Chunya mkoani Mbeya wakiwa na mali za wizi ambazo ni bidhaa mbalimbali za dukani pamoja na Sh. milioni 1.3 kati ya Sh. milioni 2.8 walizoiba.

Alidai watuhumiwa walikutwa na gari yenye namba T.571 DXS aina ya Nissan X Trail rangi nyeusi ambayo hutumia katika uhalifu wao.

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa walihojiwa na kukiri kufanya matukio ya uhalifu katika maduka na mawakala wa fedha katika mikoa mbalimbali nchini.



Mtaalamu wa Elimu ya Ujasiriamali kutoka Shirika la Envirocare linalojihusisha na kilimo cha kahawa na jinsia, Grace Muro, akitoa elimu ya utengenezaji wa sabuni kwa kutumia malighafi za kahawa kwa wajasiriamali (hawapo pichani), wa kijiji cha Mlowo, Kata ya Isuto wilayani Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Kampuni ya ununuzi kokoa kutoa elimu kwa wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

KAMPUNI ya ununuzi wa kokoa katika Wilaya za Kyela na Rungwe mkoani Mbeya, imeihakikishia serikali kuendelea kutoa elimu katika sekta ya afya kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema ili kuendelea kuzalisha kwa tija.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Bioland Intenational Ltd, Fons Maex, alisema katika kufanikisha hayo zaidi ya vitabu 50,000 vya masomo ya kiingereza na hisabati vimetolewa kupitia programu ya cocoa for schools kwa shule za msingi zilizopo katika Halmashauri ya Busokelo na Rungwe mkoani Mbeya.

Alisema mbali na kutoa vitabu hivyo kukabiliana na tatizo la ukosefu wa vitabu shuleni, lakini wana lengo la kuongeza ufaulu wa masomo ya hisabati na kiingereza kutokana na wanafunzi kufanya vibaya katika masomo hayo.

Lengo la utoaji wa vitabu hivyo ni kukabiliana na uhaba wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia kwa masomo ya hisabati na kiingereza.

"Zaidi ya Sh. milioni 30 zimetumika kununua vitabu hivi ambavyo naamini vitaongeza ufaulu kwa watoto wetu maana tulibaini miongoni mwa sababu zinazochangia kufanya vibaya kwenye masomo hayo ni uhaba wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia," alisema Maex.

Aidha, Maex aliwataka walimu wa shule za msingi katika Halmashauri ya Busokelo na Rungwe kuongeza bidii ya kufundishia watoto ili mitihani ijayo halmashauri hizo ziwe kinara.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema licha ya serikali kuboresha miundombinu ya shule ikiwamo vyumba vya madarasa, vyoo na baadhi ya vifaa vya maabara bado kuna uhitaji mkubwa wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia hususani kwenye masomo ya sayansi.

Alisema kwa sasa mazingira ya mwanafunzi kukaa shuleni yatakuwa mazuri na yatamvutia kwani atakaa kwenye mazingira safi na kujisomea kwa utulivu ili kutimiza ndoto zake.



# Dk. Mwinyi aagiza Barabara Charawe-Ukongoroni kujengwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemaliza kero ya miaka mingi iliyokuwa ikiwasibu wananchi wa Charawe na Ukongoroni Mkoa wa Kusini Unguja, kwa kuagiza kujengwa barabara katika eneo hilo.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliwasilisha salamu hizo za Rais jana wakati akizungumza na wananchi wa Ukongoroni na Charawe.

Aidha, Waziri Dk. Khalid alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 22 itajengwa na Kampuni ya ORKUN kutoka nchini Uturuki na itakuwa na ukubwa mita tisa upana na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi minne.

"Nawahakikishia ndugu wananchi kampuni hii ina uwezo mkubwa sana wa kila hali kwani ndio iliyopewa kazi kujenga reli ya SGR nchini," alieleza.

Hata hivyo aliwataka wananchi kuondoa shaka juu ya utendaji kazi wa viongozi wa juu akisema wanatekeleza kila ambacho wamekiahidi.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid, alimpongeza waziri huyo kwa ujasiri wake kwa kuichukua changamoto hiyo na ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na kutoa mrejesho kwa wananchi.



**Dk. Hussein Ali Mwinyi, amemaliza kero ya miaka mingi iliyokuwa ikiwasibu wananchi wa Charawe na Ukongoroni Mkoa wa Kusini Unguja, kwa kuagiza kujengwa barabara katika eneo hilo.**

# 'Wazanzibar wanufaika na rasilimali za bahari'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema wakazi wa Zanzibar wanaendelea kunufaika na rasilimali za bahari katika nyanja za uchumi.

Aliyasema hayo jana Mkoa wa Kaskazini Unguja, wakati akifungua semina ya kujadili uratibu wa uchumi wa buluu kwa mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema kukamilika kwa sera na mpango mkakati wa uchumi wa buluu kutatoa fursa zaidi kwa Wazanzibar kunufaika na uchumi, hivyo aliwataka wavuvi kuendelea kuhifadhi mazingira ya bahari kwa manufaa ya baadaye.

Hamza alisema Zanzibar imezungukwa na bahari, hivyo ni muhimu kutekeleza mipango ya sera kupitia dhana ya uchumi wa buluu ili Wazanzibari wafaidike na uchumi huo.

**Hiyo ndiyo njia ya kuinua mnyororo wa thamani ya sekta ya uchumi wa buluu na kufungua milango mipya ya masoko ya kisasa na kimataifa ya bidhaa za uchumi wa buluu.**

Alisema Zanzibar ina uzoefu wa mifumo ya usimamizi mzuri wa sera za kitaifa ikiwamo usimamizi wa sera za maafa na usimamizi wa sera ya uhakika wa chakula na lishe.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema ili dhana ya uchumi wa buluu ifikiwe lazima kuimarisha sekta ya za elimu, ubunifu, nyenzo, fursa za mitaji, masoko, kuimarisha usawa wa kijinsia na jamii, ubora wa bidhaa, ulinzi na usalama wa mazingira ya bahari pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, alisema serikali inaendeleza kuweka mazingira bora ya uwekezaji, kurahisisha biashara kutatua matatizo mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji bora wa mpango wa maendeleo wa Zanzibar (ZADEP).

"Hiyo ndiyo njia ya kuinua mnyororo wa thamani ya sekta ya uchumi wa buluu na kufungua milango mipya ya masoko ya kisasa na kimataifa ya bidhaa za uchumi wa buluu," alisema.

Mwakikishi kutoka Shirika la Uhifadhi wa Wanyama pori (WWF) Tanzania, Matrida Simfukwe, alisema uchumi wa buluu ni miongoni mwa nyanja muhimu za kuangazia katika suala zima la uhifadhi na manufaa ya rasilimali za bahari.

Wakichangia mada kuhusu muundo wa sera ya uchumi wa buluu mawaziri hao waliitaka serikali kuwa makini juu ya utumiaji wa bahari hasa kwa wananchi na wawekezaji, kuondoa changamoto inayoweza kujitokeza hasa katika matumizi ya ufukwe.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto), akizungumza na Mzee Fumu Fadhili Makame wa Shaurimoyo, wakati wa ziara yake ya kuwajulia hali wagonjwa, wazee na wananchi wenye changamoto mbalimbali kisiwani humo juzi. **PICHA: OMKR**

# Viongozi watakiwa kuwa karibu na wananchi wakati wa mfungo

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni wajibu kwa viongozi kuwa karibu na wananchi ili kusaidia kujenga umoja na ushirikiano hasa katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Othman ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Zanzibar, aliyasema hayo jana Unguja baada ya kukamilisha ziara yake ya kutembelea wagonjwa na wajane katika majimbo mbalimbali ya Uguja na Pemba.

Othman alisema ziara kama hizo ni muhimu na zinasaidia viongozi kupata funzo la kufahamu hali na maisha ya watu yalivyo na kutafakari juu ya namna bora ya kuendeleza umoja.

"Ziara kama hizi pia zinatoa nafasi kwa viongozi kusikiliza moja kwa moja matatizo ya wananchi na kuweza kufahamu, hivyo kuwezesha kutafakari namna ya kutafuta mbinu za pamoja za kuyatatua,"alisema.

Hivyo aliwataka waliopatwa na mtihani wa maradhi ya aina mbalimbali kuendelea kuwa na subira na kufahamu kwamba maradhi ni mtihani kutoka kwa Mungu.

Katibu wa Haki za Binadamu na Makundi Maalum wa ACT - Wazalendo, Pavu Abdalla Juma, alisema ziara hizo ni mwendelezo wa urithi muhimu kutoka kwa mtangulizi wake Hayati Maalim Seif Shariff Hamad ambazo alizifanya kila ifikapo Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na zinasaidia katika kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi na viongozi wao.

Katibu wa ACT- Wazalendo Mkoa wa Mjini Magharib, Mahamoudu Ali Mahinda, alisema chama hicho katika ngazi ya Mkoa wa Mjini kimeanzisha mfuko maalum wa faraja kwa ajili ya kusaidia wenye shida na changamoto mbalimbali.

Othman katika ziara hiyo alitembelea majimbo ya Chumbuni, Shaurimoyo, Amani, Magomeni, Kwahani, Mpandae, Jang'ombe, Kiwajuni na Malindi katika Wilaya ya Mjini Unguja.

# Wanahabari wanaoripoti matukio ya maandamano washambuliwa Kenya

**NAIROBI, Kenya**

WANAHABARI wa ndani na wa kimataifa wanaofuatilia maandamano nchini Kenya wameshambuliwa na wengine kujeruhiwa baada ya genge la watu wenye visu kurushia magari yao mawe wakiwa katika eneo la Kibra, licha ya polisi kutanda kila kona kuzuia ghasia hizo.

Wiki iliyopita kiongozi mkuu wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga, aliitisha maandamano mara mbili kila wiki Jumatatu na Alhamisi, kwa lengo la kupinga serikali juu ya kupanda kwa gharama za maisha.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani, Jase Ndung'u, mwandishi wa habari anayefuatilia maandamano katika eneo la Kibra, alieleza kuwa genge lililojihami liliwavamia wanahabari waliokuwa wakifuatilia maandamano hayo, na kuwalazimisha kukimbia kuokoa maisha yao.

"Genge hilo lilijifanya kuwa sehemu ya waandamanaji lakini walikuwa na silaha," alisema Ndung'u.

Ilielezwa kuwa wanahabari walilazimika kutoroka genge la watu wenye visu kwenye gari la luninga ya Citizen huko Kibra, Nairobi, na kwamba baadhi ya waandishi wamepoteza simu zao, pochi na vitu vingine vya thamani.

Alisema polisi walifyatua gesi ya kutoa machozi kutawanya maandamano baada ya upinzani kuapa maandamano yataendelea licha ya marufuku ya polisi.

Taarifa zilisema usalama uliimarishwa, huku polisi wa kutuliza ghasia wakiwa katika maeneo ya kimkakati jijini Nairobi na kushika doria mitaani, maduka mengi yakiwa yamefungwa na huduma za treni kutoka viunga vya mji mkuu hadi wilaya kuu ya biashara zilisitishwa.

Kinara wa upinzani Odinga, alitoa wito kwa watu kujitokeza barabarani hata baada ya maandamano ya wiki jana ambayo yalisababisha vurugu na kusimamisha shughuli katika baadhi ya sehemu za mji wa Nairobi.

Aidha, ilielezwa kuwa askari wa kutuliza ghasia nchini Kenya walitanda katika mitaa ya mji mkuu, Nairobi, katika jitihada za kuzuia maandamano yaliyoitishwa na upinzani kuhusu gharama ya juu ya maisha na madai ya ukiukwaji wa maadili katika uchaguzi.

Viliripoti kuwa maduka yalifungwa katikati mwa jiji la Nairobi huku wamiliki wa biashara wakihofia uporaji.

Katika mji wa magharibi wa Kisumu, ngome ya upinzani, vitoa machozi vilirushwa kutawanya umati wa waandamanaji waliokuwa wakiongozwa na gavana wao wa eneo hilo.

Polisi walisema watawapiga picha waandamanaji na kuwafungulia mashtaka kwa kushiriki maandamano haramu.

***BBC***




Polisi nchini Kenya wakiimarisha doria kuzuia maandamano katika baadhi ya maeneo. **PICHA: MTANDAO**

# Jumuiya ya kimataifa yamkosoa Putin

**MASCOW, Russia**

JUMUIYA ya kimataifa na washirika wa nchi za magharibi wameukashifu mpango wa Rais wa Russia, Vladmir Putin wa kutaka kuhifadhi silaha zake za kimkakati za nyuklia huko Belarus.

Rais Putin alitangaza Jumamosi ya wiki iliyopita kuwa, nchi yake itaweka silaha za kivita za nyuklia huko Belarus hatua aliyoitaja kuwa ni sawa na Marekani ilivyohifadhi silaha kama hizo katika mataifa kama Ujerumani, Ubelgiji na Uturuki.

Ilielezwa kuwa tangazo hilo ni moja ya ishara za nyuklia zinazotolewa na Russia na onyo kwa jumuiya ya kujihami ya NATO dhidi ya uungaji mkono wake wa kijeshi kwa Ukraine, iliyotaka kuitishwa kwa mkutano wa dharura wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kujibu hatua hiyo ya Russia.

Msemaji wa NATO, Oana Lungescu, alisema kwamba Russia mara kwa mara imekuwa ikivunja ahadi zake kuhusu udhibiti wa silaha zake za kimkakati za nyuklia, na kwamba jumuiya hiyo ipo inafuatilia kwa ukaribu hatua za Russia.

Lithuania, nayo imeweka bayana kutoa vikwazo vipya kwa Moscow na Minsk endapo mpango huo utatekelezwa.

Tangazo hilo la Russia lililoongeza hofu juu ya vita vya nyuklia kwa mujibu wa wataalamu, pia limelaaniwa vikali na Umoja wa Ulaya (EU) ulioitaka Belarus kutoshiriki mpango huo.

Mkuu wa sera za kigeni wa EU Josep Borrell, alisema Belarus kukaribisha silaha za nyuklia za Russia kunaweza kumaanisha kuongezeka kwa kutowajibika na tishio kwa usalama wa Ulaya na kwamba Umoja huo upo tayari kujibu kwa vikwazo zaidi.

Hata hivyo, Marekani ambayo nayo ni miongoni mwa mataifa yanayomiliki silaha za kimkakati za nyuklia imepuuza juu ya mpango wa Russia kupeleka silaha hizo Belarus.

Msemaji wa Ikulu ya Marekani, Johnn Kirby, alisema hawajaona dalili zozote kwa Rais Putin kujiandaa katika kutumia silaha hizo. "Pia naweza kusema kuwa hatujaona chochote ambacho kingetufanya kubadili mkakati wetu wa kuzuia nyuklia," alisema Kirby.

Ilibainishwa kuwa Belarus na Russia zina uhusiano wa karibu kijeshi na Minsk iliruhusu Moscow kutumia eneo la Belarus kama kituo cha uvamizi wake kamili wa Ukraine mwaka jana.

***DW***

## Uganda yapigilia msumari sheria kupinga ushoga

**KAMPALA, Uganda**

WAZIRI wa Habari wa Uganda, Dk. Chris Baryomunsi, amesema kwamba Rais wa nchi hiyo Yoweri Museveni, atasaini muswada uliopitishwa na bunge unaoharamisha ushoga nchini humo, na kuwa sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Baryomunsi alisisitiza kuwa Museveni atasaini muswada huo, huku akionya jumuiya ya kimataifa dhidi ya kile alichotaja kama kuwatisha viongozi wa Uganda kwamba watawekewa vikwazo.

"Tunatunga sheria kwa ajili ya raia wa Uganda na wala sio wazungu, kama wanataka, basi watuwekee vikwazo," alisema Baryomunsi.

Inaelezwa kuwa mashirika ya kutetea haki za kibinadamu yamekashifu hatua ya bunge la Uganda kupitisha muswada unaoharamisha ushoga nchini humo, yakisema ni ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu.

Muswada uliopitishwa na bunge una hukumu ya hadi kifo kwa wanaofanya mapenzi ya jinsia moja na kuambukiza wengine virusi vya ukimwi.

Kwa mujibu wa muswada huo, watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja watahukumiwa miaka 20 gerezani, huku wale watakaopatikana wakijaribu kufanya jambo hilo wakihukumiwa miaka 10 gerezani.

Waziri wa sheria na masuala ya katiba wa Uganda Nobert Mao, alitoa wito kwa raia wa Uganda kukataa kile alichokitaja kama jaribio la kuharibu mila na tamaduni zao.

"Wakati mwingine, hawa watu wanaoitwa wafadhili, jumuiya ya kimataifa na wanaotutishia, hawatutakii mema," alisema Mao.

Mao aliongeza kwamba itakuwa vigumu kwa mataifa ya magharibi kukubali mataifa ya Afrika kupeleka utamaduni wao katika mataifa hayo na kuhoji kinachosababisha kulazimisha ushoga kwa mataifa mengine.

***VOA***

**"Tunatunga sheria kwa ajili ya raia wa Uganda na wala sio wazungu, kama wanataka, basi watuwekee vikwazo," alisema Baryomunsi.**

# AZAM, GOR MAHIA BASI TENA, KUKIWASHA NA KMC FC LEO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imetangaza rasmi kuwa haikwenda nchini Kenya kucheza mechi yake ya kirafiki dhidi ya Gor Mahia kama ilivyopangwa kutokana na hali ya kisiasa nchini humo kutokuwa shwari.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia maarufu 'Zaka Zakazi', amesema awali ilipangwa mechi hiyo ingechezwa jana kwenye Uwanja wa Nyayo, Nairobi nchini Kenya, lakini imeshindikana kutokana na sababu za hali ya kisiasa inayoendelea nchini humo kati ya serikali na wafuasi wa aliyekuwa mgombea wa kiti cha Urais, Raila Odinga.

Kutokana na hali hiyo, timu hiyo itacheza mechi yake ya kirafiki leo Jumatatu saa 3:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, dhidi ya KMC ya Kinondoni.

"Tutacheza na KMC leo, awali tulipanga kucheza na Gor Mahia, mechi ilikuwa ifanyike Jumapili Uwanja wa Nyayo, Nairobi nchini Kenya, lakini hali ya kisiasa nchini humo kwa sasa si nzuri ikabidi tutafute timu nyingine na kwa muda mfupi uliopatikana timu yenyewe ilikuwa ni hii KMC, kwanza tumeshamalizana nao mzunguko wa pili, timu zingine ni kama tumezishtukiza sana hazikuwa na muda.

"Lakini baadhi zinatuogopa zinaona tukikutana nao saa hizi  tutawazoea halafu kwenye mechi za mzunguko wa pili itakuwa matatizo, lakini kwa KMC wenyewe nao wanauhitaji kwa sababu wapo kwenye kipindi kigumu katika msimamo wa Ligi Kuu, hivyo mechi hiyo ni muhimu kwao," alisema.

Alisema baada ya mechi dhidi ya Gor Mahia kugonga mwamba kuchezewa nchini Kenya, walifikiri kuileta Tanzania, lakini muda ukakwamisha kwani ukawa mdogo kwa kila timu kuendelea na programu zake.

"Tulifikiria kama kuileta Gor Mahia kucheza nchini, lakini muda umekuwa mfupi sana, badala yake tuna mechi hii kwa sababu wachezaji wakikaa muda mrefu utimamu wa mwili unapungua, hivyo ni lazima utengeneze mechi hapo katikati ili kulinda ule utimamu wao," alisema.

Azam itacheza mechi hiyo ikiwa ni maandalizi ya mchezo wao wa robo fainali wa Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) maarufu Kombe la FA dhidi ya Mtibwa Sugar, utakaopigwa Uwanja wao wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

# New City, Ngome FC zapanda Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JUMLA ya timu nne kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, zimeshuka daraja, hivyo msimu ujao zitacheza Ligi ya Mikoa zilipotoka.

Ligi Daraja la Kwanza Zanzibar tayari imemalizika huku timu ya New City na Ngome FC zikishuhudiwa kupanda daraja kutokea Kanda ya Unguja ambapo zitaungana na nyingine mbili kutoka Kanda ya Pemba kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Kwa upande wa timu ambazo zimeshuka daraja kwa msimu huu ambazo zitakwenda kucheza Ligi ya Mikoa msimu ujao, ni Jang'ombe Boys, Chuoni FC na Gulioni FC zitakwenda kucheza Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi wakati timu ya Strong Fire FC itakwenda kucheza Ligi ya Mkoa wa Kusini Unguja.

Hata hivyo, kwa mujibu wa kanuni ya mashindano msimu huu wa 2022/23, jumla ya timu sita zitapanda daraja kutoka katika mikoa mitatu ya Unguja na kwenda kucheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kwa msimu ujao.

Kwa mkoa wa mjini, tayari timu mbili zilizopanda ni Negro United na Mambuu FC, na kwa upande wa Kaskazini ni timu ya Sharb Boys na Sulubu FC, hivyo bado timu mbili kutoka Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema kwa upande wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imemaliza kwa mafanikio makubwa kama walivyotarajia kwa mujibu wa ratiba.

Alisema zipo changamoto kadhaa ambazo zimejitokeza kwa baadhi ya michezo ikiwamo changamoto ya viwanja hasa kwa vile viwanja vya mikoani.

Hata hivyo, alisema baada ya mwezi wa Ramadhani wanatarajia kukaa kikao  cha pamoja kufanya tathmini ya ligi hiyo.

**UNANIELEWA?...**



Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Adel Amrouche, akitoa maelekezo kwa Ibrahim Bacca huku  Novatus Dismas (kulia) naye akisikiliza kwa makini, wakati wa mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, dhidi ya Uganda itakayopigwa uwanjani hapo leo usiku. **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kutia mkono gofu

**Na Shufaa Lyimo**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, imesema itatumia nguvu nyingi kuwekeza kwenye michezo yote nchini ukiwamo wa gofu ili kuondoa dhana kuwa mchezo unaungwa mkono zaidi nchini ni mpira wa miguu.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam juzi usiku na Naibu Waziri wa  Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', wakati akifunga shindano la NBC Lugalo Open 2023.

"Wizara imejipanga kuinua michezo yote hapa nchini kwa lengo la kuitangaza nchi yetu kupitia michezo, ili kuunga mkono juhudi za rais wetu kwa vitendo," alisema Mwinjuma.

Aidha, waziri huyo alipongeza Klabu ya Gofu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Lugalo (TPDF), kutokana na juhudi wanayoifanya kuibua vipaji kwa upande wa vijana, pamoja na kuruhusu raia kushiriki mashindano katika viwanja vyao.

Pia aliishukuru Benki ya Taifa ya Biashara NBC kutokana na kazi kubwa wanayoifanya ya kudhamini michezo mbalimbali ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara na kuzitaka taasisi nyingine ziige mfano huo.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Brigedia Jenerali  Mstaafu, Michael Luwongo, alisema klabu hiyo ni miongoni mwa klabu inayoofanya vema katika mchezo huo.

Alisema shindano hilo lililomalizika  lilishirikisha wachezaji 150 kutoka klabu zote za gofu Tanzania na kuwapongeza washindi wote.

Katika shindano hilo mshindi wa jumla alikuwa ni Ally Isanzu kutoka   Klabu ya TPC Moshi mkoani Kilimanjaro, ambaye amepata makombe mawili pamoja na zawadi ya friji, huku upande wa wanawake akiwa ni Hawa Wanyeche, aliyezawadiwa jiko la umeme pamoja na kombe.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RAMOS ATAKIWA UNITED**
KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Benfica na Ureno, Goncalo Ramos mwenye umri wa miaka 21, ambaye ana kipengele cha kuondoka cha euro milioni 120. ***(Record, via Goal)***

**BUSQUETS ANUKIA MAREKANI**
KIUNGO wa kati wa Hispania, Sergio Busquets, mwenye umri wa miaka 34, bado hajakubali mkataba mpya na Barcelona na anaweza kuhamia Ligi Kuu ya Marekani. ***(Mundo Deportivo)***

**ONANA ALENGWA ARSENAL**
CHELSEA na Arsenal zitamenyana katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuanza vema soka lake pale Goodison Park. ***(Fichajes)***

**RAYA KUMRITHI DE GEA**
MANCHESTER United watamfikiria kipa wa Brentford, David Raya, mwenye umri wa miaka 27, kama mbadala wa David de Gea (32), ambaye bado hajakubali kusaini mkataba mpya. ***(Give Me Sport)***

**OSIMHEN AWINDWA CHELSEA**
CHELSEA iko tayari kutoa euro milioni 100 kumnunua mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Napoli. (Football Insider)

**CAICEDO KIPAUMBELE ARSENAL**
ARSENAL itaweka kipaumbele jaribio lingine la kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21 kuelekea msimu wa majira ya joto. ***(Football transfers)***

**KANTE KUONGEZA MKATABA**
CHELSEA iko kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 31, kuhusu mkataba mpya wa miaka miwili, kukiwa na chaguo la mwaka zaidi Stamford Bridge. ***(Fabrizio Romano)***


**CHAMBERLAIN ATAKIWA VILLA**
ASTON Villa, Newcastle na Brighton wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa England, Alex Oxlade-Chamberlain, mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake na Liverpool unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

**NEVES BASI TENA BARCA**
BARCELONA imejiondoa katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Ureno na Wolves, Ruben Neves, mwenye umri wa miaka 26, msimu huu. ***(Fichajes)***

**TUCHEL KUIBOMOA CHELSEA**
KLABU ya Chelsea imesikitishwa na kocha wao wa zamani, Thomas Tuchel, kwa kuweka hadharani nia yake ya kumchukua Anthony Barry kwenda Bayern Munich. ***(Telegraph)***

**FERGUSON AIKATAA UNITED**
MSHAMBULIAJI Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 18, atakataa kuhamia Manchester United kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Ireland anadhani kusalia Brighton kutakuwa bora zaidi kwa maendeleo yake. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES HAKUBALIANI NA RONALDO 'HEWA SAFI' URENO

**Hali katika timu ya taifa daima imekuwa nzuri, hakujawahi kuwa na kitu chochote ambacho hakikuwa...**

**LISBON, Ureno**

BRUNO Fernandes haamini Ureno ilihitaji "pumzi ya hewa safi" ambayo Cristiano Ronaldo alikuwa anatazamia chini ya Roberto Martinez.

Martinez amechukua mikoba ya Ureno kwa mara ya kwanza katika mapumziko haya ya kimataifa, kutokana na kumrithi Fernando Santos baada ya Kombe la Dunia.

Kocha huyo wa zamani wa Ubelgiji amesimamia ushindi wa mabao 4-0 na 6-0 dhidi ya Liechtenstein na Luxembourg katika michuano ya kufuzu Euro 2024.

Nahodha wa Ureno, Ronaldo alifunga mara mbili katika kila mechi, baada ya kuzungumza juu ya "hewa safi sasa, mawazo tofauti " huku Martinez akiongoza usukani.

Licha ya mwanzo mzuri, hiyo si tathmini ambayo Fernandes anakubaliana nayo.

"Hapana, ni kocha mpya mwenye mawazo mapya," kiungo huyo wa kati wa Manchester United aliiambia RTP3 baada ya ushindi wa Jumapili dhidi ya Luxembourg.

"Hakuna pumzi ya hewa safi kabisa. Ni kipindi cha mpito tu.

"Hali katika timu ya taifa daima imekuwa nzuri. Hakujawahi kuwa na kitu chochote ambacho hakikuwa safi, kwa hivyo nadhani ni mwenendo mpya tu, kocha mpya, na unapaswa kuiga mawazo yake."

Fernandes alichezeshwa mechi yake ya kwanza ya Ureno na Santos, ambao alikuwa amewaongoza 'Selecao' kushinda taji la Euro 2016.

Santos aliondoka baada ya kutolewa kwa mshtuko robo fainali mikononi mwa Morocco kule Qatar 2022.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,093,3
MECHI KALI
SPAIN
NORWAY
1 | 1.40
X | 4.64
2 | 8.20
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
*150*87#

# CONTE AACHANA NA TOTTENHAM



**LONDON, England**

ANTONIO Conte ameondoka Tottenham Hotspur kwa makubaliano baada ya kuiongoza kwa miezi 16, klabu hiyo imetangaza.

Spurs wako nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, lakini hawatamaliza kungoja kwa miaka 15 kwa kombe msimu huu baada ya kutoka kwenye mashindano yote.

Msaidizi wa Conte, Cristian Stellini, ameteuliwa kuwa kaimu kocha mkuu kwa msimu uliosalia huku Ryan Mason akichaguliwa kuwa msaidizi wa Stellini.

Mwenyekiti Daniel Levy alisema katika taarifa yake Jumapili jioni: "Tumebakiza mechi 10 za Ligi Kuu na tuna mapambano mikononi mwetu kuwania nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sote tunahitaji kuvuta pamoja. Kila mmoja anapaswa kujitokeza ili kuhakikisha mwisho wa juu zaidi kwa klabu yetu na wafuasi wetu waaminifu."

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Conte alikuwa amechanganyikiwa kwa kile alichoona ni tofauti katika mkakati na klabu kusita kujitolea kufanya marekebisho makubwa ya timu ambayo aliamini ni muhimu.

Wasiwasi huu umekuwa ukioneshwa mara kwa mara, lakini Conte hakuweza kuficha hasira yake kwa wachezaji baada ya kuruhusu uongozi wa mabao 3-1 kuteleza katika Uwanja wa Southampton, na kufungwa mara mbili katika dakika 15 za mwisho hivyo kutoka sare ya 3-3.

Katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi, Conte alianzisha mashambulizi makali kwa wachezaji na wamiliki wa klabu.

"Hadithi ya Tottenham ni hii: Miaka 20 kuna mmiliki huyu na hawakuwahi kushinda chochote. Kwa nini?" Conte alisema.

"Kosa ni kwa klabu tu, au kwa kila kocha anayekuja hapa? Nimeona makocha ambao Tottenham walikuwa nao kwenye benchi. Una hatari ya kuvuruga sura ya makocha na kulinda hali nyingine kila wakati.

"Hadi sasa najaribu kuficha hali hiyo, lakini si sasa hivi kwa sababu, narudia, sitaki kuona nilichokiona leo kwa sababu jambo hili halikubaliki na pia halikubaliki kwa mashabiki."

Aliendelea: "Sisi ni wachezaji 11 wanaoingia uwanjani. Naona wachezaji wenye ubinafsi, naona wachezaji ambao hawataki kusaidiana na hawaweki moyo kwa klabu.

"Kwa uzoefu wangu, naweza kuambia kwamba ikiwa unataka kuwa mshindani, ukitaka kupigana, lazima uboreshe kipengele hiki. Na kipengele hiki, naweza kukuambia, katika wakati huu ni kweli. Na mimi natazama wachezaji 11 pekee wanaocheza wenyewe.

"Wamezoea. Hawachezi kitu muhimu hapa. Hawataki kucheza kwa shinikizo, hawataki kucheza wakiwa na msongo wa mawazo."

Spurs sasa watatafuta kocha wao wa tisa tangu kushinda taji lao la mwisho, Kombe la Ligi mwaka 2008 dhidi ya Chelsea.


# Bayern yapanga kumnunua Lukaku

**MUNICH, Ujerumani**

CHELSEA wanaonekana kupata hasara kubwa kwa Romelu Lukaku, ambaye amezifumania nyavu mara tano pekee akiwa Inter Milan kwa mkopo msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti ya Football Insider, 'The Blues' hao wako tayari kumuuza mwishoni mwa msimu huu, huku Inter ikiwa na uwezekano wa kujaribu kuongeza muda wake wa kukaa naye.

Chelsea walitumia pauni milioni 97.5 kumrejesha Lukaku Stamford Bridge mnamo Agosti 2021, lakini sasa kuna uwezekano wa kumuuza



jumla.

Fichajes imedai kuwa Bayern Munich wanapanga kumnunua Lukaku ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Ripoti hiyo inadai kuwa Bayern inavutiwa na mshambuliaji huyo wa Ubelgiji, ambaye ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani iwapo anakuwa fiti bila majeraha.

Hata hivyo, Bayern haitaanza mazungumzo na Chelsea hadi mwishoni mwa msimu huu.

Mabingwa hao wa Ujerumani walikuwa wakihusishwa na Harry Kane wakitafuta mtu wa kuchukua nafasi ya Robert Lewandowski, ambaye aliondoka kwenda Barcelona mwaka jana.

Calciomercato imeripoti kwamba Chelsea wanaweza kujaribu kupata dili na Roma kwa kubadilishana mkataba unaomhusisha Tammy Abraham.

395,265/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII

MECHI ZA USHINDI

# DODOMA JIJI FC WAJIFUNGIA KUJINUSURU KUSHUKA DARAJA

**Na Adam Fungamwago**

UONGOZI, benchi la ufundi na wachezaji wa timu ya Dodoma Jiji wamefanya kikao kizito kujadili hatima ya klabu hiyo, ikiwa ni kufanya mikakati na kutoa hamasa kwa ajili ya kuinusuru timu hiyo kwenye janga la kushuka daraja.

Meneja wa klabu hiyo, Charles Komba, amesema katika kikao chao wamejipanga kuhakikisha wanashinda mechi kuanzia ile watakayocheza dhidi ya Coastal Union Aprili 16, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Komba alisema maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekuwa makubwa zaidi na kila mmoja ana ari ya ushindi.

"Tumejipanga kuhakikisha tunashinda, tunaanza na mechi dhidi ya Coastal Union, halafu tuangalie zinazofuata, maandalizi kwenye mechi hii yawepo vizuri kwa uongozi," alisema meneja huyo.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Kassim Liogope, amesema kikosi chao kimerejea mazoezini baada ya wiki moja ya mapumziko kwa wachezaji na sasa macho yote yanaelekezwa kwenye mechi hiyo dhidi ya Coastal.

"Tumejipanga kukabiliana na Coastal Union nyumbani, lakini lengo ni kuhakikisha mechi zetu zote tano tunafanya vizuri, tunajua hatupo kwenye nafasi nzuri, ingawa nafasi tuliyonayo ni tofauti na tuliyokuwa nayo huko nyuma, tulikuwa chini sana na kusema kweli ligi ni ngumu.

"Kwa hiyo kikubwa tumejipanga kuhakikisha tunashinda mechi zetu mbili za nyumbani, kwa sasa tunajadili na yule aliye karibu yetu, sasa hivi tunamwangalia Coastal ambao mechi ya mzunguko wa kwanza tulikwenda kumfunga kwake, kwa sasa tuko nyumbani, kwa vyovyote watakuja kwa ajili ya kulipiza kisasi, lakini sisi kama Dodoma Jiji, tumejipanga kuhakikisha tunapata pointi tatu," alisema kcha huyo msaidizi.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza Novemba 30, mwaka jana, Dodoma Jiji iliichapa Coastal Union bao 1-0 katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Timu hiyo inakamata nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikikusanya pointi 27, ikiwa ni moja kati ya timu ambazo hazipo salama, zinazoweza kushuka daraja, au kwenda kucheza mechi za mchujo kama zitafanya vibaya katika mechi tano za mwisho zilizobaki.

# Taifa Stars vs Uganda 'gharika' kwa Mkapa

INATOKA UK. 24

Alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya matokeo ya mechi iliyopita dhidi ya Uganda na watakuja kivingine katika baadhi ya maeneo ili kuhakikisha wanapata ushindi.

"Tumefanya kazi kubwa kuhakikisha yale madhaifu yetu yaliyojitokeza mechi ya kwanza tunayatatua, pia kuongezeka kwa Mohamed (Hussein Tshabalala), Kapombe (Shomari) kutaongeza kitu katika kikosi," alisema Morocco.

Kwa upande wa mwakilishi wa wachezaji, Msuva alisema bado wana kazi kubwa kwa sababu hawajamaliza mechi na ushindi waliopata Misri hautawafanya kuona wamemaliza.

"Kazi kubwa iko mbele yetu, hatujamaliza na tunatakiwa kupambana kutafuta matokeo kwenye mchezo wa kesho (leo), kutafuta ushindi dhidi ya Uganda ili kujihakikishia nafasi ya kufuzu," alisema Msuva.

Aliongeza kuwa hamasa ya Rais Samia Suluhu Hassan imeongeza kitu ndani ya timu, lakini kwao muhimu ni kupambania nchini kutafuta tiketi ya kufuzu fainali hizo.

Naye Kocha wa The Cranes, Milutin Sredejovic 'Micho', alisema watahakikisha wanawazuia wachezaji wa Stars ambao wamewapa wakati mgumu akiwamo Mzamiru Yassin, Himid Mao, Mudathir Yahya na Msuva.

Alisema nyota hao walikuwa mwiba mchungu kwao kwa katika mchezo



wa kwanza nchini Misri na leo watakuwa makini kuwachunga zaidi .

"Ni mechi ngumu sana kwa sababu tunahitaji kulipa kisasi kwa kutafuta ushindi, pia ukizingatia Tanzania ni majirani zetu, nimefanyia kazi mapungufu yaliyojitkeza mechi iliyopita na hatutacheza kwa presha kubwa," alisema Micho.

Nahodha wa The Cranes, Emmanuel Okwi, alisema licha ya kupoteza mechi nchini Misri, sasa wamekuja Tanzania kwa ajili ya kusaka pointi tatu baada ya benchi la ufundi kufanyia kazi mapungufu ya mchezo uliopita.

"Ni mechi ngumu na tumekuja kupindua meza, tumepata pigo kwa kukosa mchezaji wetu mmoja nchini Misri, lakini hatutarudi nyuma kuhakikisha tunapambana kutafuta ushindi wa alama tatu zitakazotuweka katika nafasi nzuri ya kufuzu fainali za Afcon," alisema Okwi.

## Robertinho: Mfumo Simba

INATOKA UK. 24

Mabingwa nyumbani dhidi ya Vipers kwenye ushindi wa bao 1-0, mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, ikishinda mabao 3-0 na Horoya AC ikishinda mabao 7-0 iliwazima midomo waliokuwa wakimbeza kocha huyo wa zamani wa Rayon Sports ya Rwanda na Vipers ya Uganda.



# Michezo

Jumanne Machi 28, 2023
Nipashe



UKURASA 21

**Fernandes hakubaliani na Ronaldo 'hewa safi' Ureno**

# TAIFA STARS VS UGANDA 'GHARIKA' KWA MKAPA

## ●●●Uwanja kutapika mashabiki 51,545 wanunuliwa tiketi, Msuva atoa angalizo, Micho ataja wakukabwa, Okwi aonya...

**Na Saada Akida**

NI gharika! Ndivyo unavyoweza kusema zikiwa zimesalia saa chache kabla ya Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), kuikaribisha Uganda (The Cranes), katika mechi ya Kundi F ya mkondo wa pili kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023 itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku leo baada ya mashabiki 51,545 kununuliwa tiketi ili kushuhudia mechi hiyo bure.

Taifa Stars yenye pointi nne katika nafasi ya pili nyuma ya Algeria iliyopo kileleni ikiwa na alama tisa, inashuka dimbani ikihitaji ushindi kwa mara ya pili mfululizo dhidi ya Uganda ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufuzu fainali hizo kwa mara ya tatu katika historia yake baada ya kushiriki mwaka 1980 na 2019.

Hata hivyo, haitakuwa rahisi kwa Uganda yenye alama moja mkiani kwenye kundi hilo, kukubali kupoteza tena mchezo huo baada ya ule wa mkondo wa kwanza uliopigwa Misri Ijumaa iliyopita kukubali kipigo cha bao 1-0, shukrani kwa Simon Msuva aliyewaliza.

Endapo Taifa Stars ikifanikiwa kupata alama tatu katika mchezo wao leo, itafikisha pointi saba nyuma ya Algeria ambayo nayo itakuwa dimbani dhidi ya Niger yenye pointi mbili, hivyo kuhitaji ushindi katika mchezo ujao dhidi ya Waniger hao ili kufuzu.

Kuelekea mchezo huo hadi jana, wadau mbalimbali pamoja na serikali wamezesha kupatikana kwa tiketi 51,545 ambazo zinagawiwa kwa mashabiki bure ili kwenda kuipa sapoti Taifa Stars katika mchezo huo.

Baadhi ya wadau waliungana na serikali katika kufanikisha kununulia mashabiki tiketi ni pamoja na Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, ambaye amenunua tiketi 5,000, Azim Dewji amenunulia wafanyakazi wake tiketi 1,000 na Mdhamini wa Klabu ya Simba, Africarriers Ltd tiketi 2,000, lengo likiwa ni kuwezesha Watanzania kujitokeza kwa wingi kuishangilia Stars.

Akizungumzia mchezo huo jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Hemed Morocco, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wanaimani ya kuendelea kupata matokeo mazuri ya ushindi kwa kuvuna pointi tatu.

INAENDELEA UK. 23



Beki wa kulia, Somari Kapombe akiwa mazoezini jana kujiandaa na mchezo dhidi ya Uganda leo. Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala', wameitwa kuongeza nguvu katika mchezo huo baada ya kutojumuishwa ule wa awali uliopigwa nchini Misri na Stars kushinda 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Robertinho: Mfumo Simba sasa 'umetiki'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ametuma pongezi kwa wachezaji wake akisema kwa sasa wameanza kumwelewa aina ya soka ambalo yeye anataka wacheze.

Robertinho ambaye awali wanachama, mashabiki wa Simba na wa soka kwa ujumla, wakiwamo baadhi ya wachambuzi walionekana hawaelewi ni aina gani ya soka ambalo amelileta kwenye kikosi hicho, wakidai halivutii tofauti na zamani, amesema ana furaha sasa kwani kwenye mechi tatu, mbili za Ligi ya Mabingwa na moja ya Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar, timu yake ilicheza kwa ufasaha aina ya soka ambalo ameingiza falsafa zake ndani ya kikosi.

"Angalia kwa sasa naweza kuwatumia Shomari Kapombe na Mohamed [Hussein 'Tshabalala'] muda wote wanakwenda mbele kusaidia mashambulizi kwa kupiga krosi kushoto na kulia, kama mshambuliaji anakaa kwenye eneo sahihi anafunga bao kwa urahisi zaidi na hilo ndilo ninalohitaji," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa kwenye mfumo wake kwa sasa ametoka kwenye kutumia straika mmoja na kuweka wawili ili wawe wanafanya kazi ya kumalizia krosi zinazopigwa pande zote kutoka kwa mabeki wake.

"Natumia washambuliaji wawili ambao wanasubiri krosi wafunge kwa kichwa au mguu, nina furaha kwa sababu mechi tatu zilizopita, timu yangu ilicheza vema sana, wachezaji wangu wamefunga mabao mengi, hatua kwa hatua tunabadilisha mtazamo kwa sababu baada ya kufanya shambulizi zuri, unatakiwa kumalizia kwa kupiga shuti. Ni muhimu sana kupiga mashuti na kufunga, hiyo ni muhimu kwangu na kwa timu kwa jumla kwa sababu mwisho wa siku tunahitaji ushindi," alisema.

Kocha huyo alikuwa akilaumiwa kutokana na wachezaji wake kutocheza soka la kuvutia lililozoeleka kwa Simba ambalo ni la pasi za taratibu na kwenda mbele kwa pasi fupi fupi hadi langoni mwa wapinzani, lakini kwa sasa amelibadilisha na kuwa la kasi, wakishambulia kwa haraka mbele na kurejea haraka kukaba.

Awali, ilionekana bado wachezaji wa timu hiyo hawajalielewa na kuzusha minong'ono, lakini mechi ya Ligi ya

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >